
SportPesa
TZS. 823,998,440
NI YA KWAKO WIKI HII,
BETI LEO UWE MILIONEA
SPORTPESA.CO.TZ PIGA *150*87#



**Shahidi** abanwa, adai hajui kama Mbowe alikimbia nchi

UKURASA 3



**RONALDO AMEICHOKA MAN UTD**

UKURASA 22


# Nipashe

Jumatano Januari 12, 2022 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII


ISSN 0856 • Na. 0580823

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper




Ofisa Habari wa Mkoa wa Mwanza, Abel Ngapemba



Johari Shani, Uhuru Digital



Husna Mlanzi- ITV



Ofisa Habari wa Wilaya ya Ukerewe, Steven Msengi

# Mshtuko wa vifo watu 14

● **Wamo** waandishi wa habari sita, Samia, Nape wawalilia... *Endelea ukurasa 2*





Mabaki ya magari mawili aina ya Toyota Landcruiser namba STK 8140 na Toyota Hiace namba T.281 DER, baada ya kugongana katika Barabara ya Musoma-Mwanza kwenye Kijiji cha Kalemela, Wilaya ya Busega, mkoani Simiyu, jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Muuguzi adaiwa kuuawa na mume kwa mapanga, kuchomwa moto

UKURASA 3



## Mwinyi ajivunia kasi maendeleo Zanzibar

UKURASA 2

**MICHEZO** **KAZE: AZAM WALISTAHILI USHINDI** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6

HABARI KITAIFA




Rais Samia Suluhu Hassan, akivuta kitambaa kufungua rasmi Kiwanda cha Nguo cha Basra Textile Mills Ltd, jana, katika shamrashamra za maadhimisho ya miaka 58 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar. PICHA: IKULU

# Mshtuko vifo vya watu 14

**Na Mwandishi Wetu**

VIFO vya wananchi 14 wakiwamo wanahabari sita waliokuwa katika msafara wa Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Robert Gabriel, umewashtua wadau mbalimbali huku Rais Samia Suluhu Hassan akiwalilia.

Kutokana na ajali hiyo, Rais Samia katika ukurasa wake wa twiter, aliandika: "Nimeshtushwa na vifo vya watu 14 wakiwamo wanahabari sita vilivyotokea leo (jana) asubuhi baada ya gari lililokuwa katika msafara wa Mkuu wa Mkoa wa Mwanza kugongana na daladala. Poleni wafiwa, wanahabari na jamii wote. Mungu aziweke mahali pema roho za marehemu na majeruhi wapone haraka."

Naye Waziri wa Habari na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye aliandika: "Nimepokea kwa masikitiko taarifa ya ajali ya gari iliyosababisha vifo vya maofisa habari, waandishi wa habari wa Mwanza na wananchi. Natoa pole kwa familia za marehemu, waandishi wa habari wote, ndugu, jamii na marafiki, Mungu aziweke mahali pema roho za marehemu wote."

Mwenyekiti wa Taasisi ya Vyombo vya Habari Kusini mwa Afrika, Tawi la Tanzania (MISA TAN), Salome Kitomari, alitoa salamu za pole kwa wote waliopoteza maisha, na kwamba tasnia ya habari imepata pigo kwa kuondokewa na nguvu kazi ambayo ilihitajika na familia zao na jamii kwa ujumla.

Mwenyekiti wa Klabu ya Waandishi wa Habari Mkoa wa Mwanza, Edwin Soko, alisema amepokea kwa masikitiko makubwa kwa kuwa wamepoteza wana taaluma wenzao na wananchi wengine ambao walikuwa kwenye majukumu ya kujenga taifa.

**DC BUSEGA**

Mkuu wa Wilaya ya Busega, mkoani Simiyu, Gabriel Zakaria, alisema waliofariki dunia ni 14 akiwamo Ofisa Habari wa Mkoa wa Mwanza, Ofisa Habari wa Wilaya ya Ukerewe na waandishi wanne, na kwamba kuna majeruhi sita akiwamo mwandishi mmoja wa Mwanahalisi ambao wanaendelea na matibabu Hospitali ya Rufani ya Bugando.

Alisema baadhi ya majeruhi walipatiwa matibabu kwenye Kituo cha Afya Nasa wilayani Busega, baadaye walihamishiwa Hospitali ya Rufani Bugando kwa matibabu zaidi.

"Miili ya maofisa habari, waandishi na dereva tumemkabidhi Mkuu wa Mkoa wa Mwanza ambayo inapelekwa Mwanza, waliobaki akiwamo dereva wa hiace inaendelea kutambuliwa na wapendwa wao. Tunaendelea na uchunguzi kujua chanzo cha ajali na hatua zaidi zitakazochukuliwa," alisema Zakaria ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya ya Busega.

**RPC SIMIYU**

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Simiyu, Blacius Chatanda, alithibitisha kutokea kwa ajali hiyo na kuwataja waliofariki ni Ofisa Habari Mkoa wa Mwanza, Abel Ngapemba, Ofisa Habari Wilaya ya Ukerewe, Steven Msengi, Anthony Chuwa (mwandishi wa kujitegemea),

Wengine ni Husna Milanzi (ITV), Johari Shan (Uhuru Digital) na dereva wa gari lililokuwa limewabeba, Paul Siang'.

Waandishi wawili walio mahututi Van Charles (Icon Blog) na Tunu Herman (Mwanahalisi Oline), wanaendelea na matibabu Hospitali ya Rufani ya Bugando.

Miili ya marehemu imehifadhiwa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Mwanza.

Akizungumzia ajali hiyo, alisema gari iliyobeba waandishi aina ya Landcruizer lenye namba za usajili STK 8140 ilikuwa kwenye mwendokasi ikitokea Mwanza kuelekea Ukerewe kupitia Bunda, ilikwepa basi la Batiko lililotokea Musoma kwenda Mwanza na kukutana uso kwa uso na hiace yenye namba za usajili T 281 DER iliyotokea Lamadi Simiyu kwenda Mwanza.

Alisema ajali ilitokea saa 12:45 asubuhi na chanzo ni mwendokasi wa gari ya Landcruizer iliyokuwa imebeba waandishi.

**RC SIMIYU**

Mkuu wa Mkoa wa Simiyu, David Kafulila, alitoa pole kwa wafiwa huku akisema ni ajali mbaya na kuwaomba wananchi kuwa watulivu na kwamba miili ya watu sita iliyokuwa sehemu ya msafara wa RC Mwanza imetambuliwa na aliondoka nayo, na ndugu wanaendelea kutambua miili minane iliyobaki.

Alisema kati ya waliofariki wanawake ni watano na wanaume tisa na kwamba chanzo cha ajali ni mwendokasi wa gari ya serikali iliyogonga ubavuni hiace ya abiria iliyokuwa umbali wa mita 38.

Kwa mujibu wa Kafulila, madereva wote wamefariki kwenye ajali hiyo na taarifa ya uchunguzi wa ajali itapatikana baada ya Kamati ya Usalama mkoa kupokea taarifa ya uchunguzi wa ajali hiyo.

**ASIMULIA ALIVYO NUSURIKA**

Mwandishi wa gazeti hili, Neema Emmanuel, alisema alipaswa kuwapo kwenye ziara hiyo, lakini alipitiwa na usingizi na kuachwa kwenye msafara huo.

"Juzi nilipigiwa simu na Ngapemba (Ofisa Habari wa mkoa, ambaye sasa ni marehemu) kuwa niwepo kwenye ziara hiyo, lakini nilipitiwa na usingizi nikaachwa na gari, hadi sasa sielewi, nimeumia sana," alisema huku akibubujikwa machozi.

## MIAKA 58 MAPINDUZI:

# Mwinyi ajivunia ongezeko mapato

**Na Gwamaka Alipipi**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi amejivunia mafanikio lukuki katika kipindi cha mwaka mmoja wa uongozi wake, ikiwamo ongezeko la mapato.

Alisema katika kipindi cha Januari hadi Novemba, mwaka jana serikali imefanikiwa kukusanya Sh. bilioni 745.1 sawa na ongezeko la asilimia 22, ikilinganishwa na makusanyo ya Sh. bilioni 610.5 zilizokusanywa kipindi kama hicho mwaka 2020.

Akizungumza wakati wa kilele cha sherehe za Maadhimisho ya Miaka 58 ya Mapinduzi ya Zanzibar, Dk. Mwinyi, alisema ongezeko hilo limechangiwa na kuimarika kwa uchumi pamoja na kuanza kutumika kwa mifumo ya kielektroniki ya ukusanyaji wa mapato iliyoanzishwa.

Dk. Mwinyi alisema mifumo hiyo inaziunganisha taasisi mbali mbali za serikali, baina ya serikali na wafanyabiashara.

Alisema sababu nyingine ni serikali kufanya marekebisho ya sheria za kanuni za kodi kwa lengo la kuondoa malalamiko ya kuwapo kwa utitiri wa kodi na ada.

Dk. Mwinyi alisema: "Ni matumaini yangu kwamba, hatua hiyo itashajihisha ulipaji wa kodi kwa hiari, kukuza ajira na kuongeza usimamizi na ukusanyaji wa mapato ya serikali."

Alisema sababu nyingine ni marekebisho ya sheria yaliyofanywa kusaidia kutoa unafuu wa ushuru wa stempu kwa wafanyabiashara wadogo na wakati kwa kupunguza viwango maalumu.

Alisema viwango hivyo ni kutoka Sh. 200,000 hadi Sh.100,000, kutoka Sh.732,000 hadi Sh. 200,000 pamoja na kupunguza kiwango cha ushuru wa stempu kutoka asimilia tatu hadi asilimia mbili kwa mwaka.

**UWEKEZAJI**

Kuhusu uwekezaji, Dk. Mwinyi alisema katika kipindi cha Novemba 2020 hadi Desemba 2021, Serikali ya Zanzibar kupitia Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji Zanzibar (ZIPA), ilisajili miradi 120 yenye mtaji wa Dola za Kimarekani milioni 787. Alisema miradi hiyo inatarajiwa kutoa zaidi ya ajira 7,000.

**UTALII**

Dk. Mwinyi alisema juhudi za serikali zimewezesha kuongeza idadi ya watalii kutoka 260,644 mwaka 2020 hadi kufikia 393,512 mwaka 2021, likiwa ni ongezeko la asilimia 50.97.

"Idadi ya kampuni za ndege zinazofanya safari kuja Zanzibar imeongezeka kutoka 27 hadi 34. Ndege hizo zilizoongezeka zinakadiriwa kuleta zaidi ya watalii 50,000 kwa mwaka," alisema Rais Mwinyi.

**VIWANDA**

Dk. Mwinyi alisema mchango wa sekta ya viwanda katika Pato la Taifa umeongezeka kutoka asilimia 18.1 mwaka 2020 hadi asilimia 19.6 mwaka 2021.

Alisema katika mwaka 2021, viwanda sita vilizinduliwa na vitatu kuwekewa mawe ya msingi. Viwanda hivyo vinatarajia kutoa wastani wa ajira 400.

**UCHUMI WA BLUU**

Dk. Mwinyi alisema serikali imeshakamilisha na kutunga sheria ya sera muhimu kwa maendeleo ya uchumi wa bluu.

Alisema serikali imeandaa mpango endelevu wenye thamani ya Sh. bilioni 149 kwa ajili ya kuwawezesha wadau wa sekta ya uchumi wa bluu wakiwamo wavuvi na wafugaji wa mazao ya baharini.

**KILIMO**

Dk. Mwinyi alisema katika sekta ya kilimo serikali imetekeleza kwa asilimia 85, mradi wa ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji katika hekta 1,053 kwa mabonde sita ya Unguja na Pemba.

**HUDUMA ZA JAMII**

Kadhalika, alieleza uimarishaji wa huduma za jamii zikiwamo elimu, afya na majisafi na salama ni miongoni mwa vipaumbele vya serikali katika kuhakikisha wananchi wa Zanzibar wanapata huduma hizo.

HABARI KITAIFA

## Shahidi adai hafahamu Mbowe alikimbia nchi

**Na Kulwa Mzee**

SHAHIDI wa nane katika kesi ya ugaidi inayomkabili Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe na wenzake watatu, Mrakibu wa Polisi (SP) Jumanne Malangahe, amedai hafahamu nani alimwambia Rais Samia Suluhu kwamba Mbowe alikuwa anajua anashtakiwa kwa ugaidi akakimbia nchini kukwepa upelelezi.

SP Jumanne alidai hayo jana Mahakama Kuu Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi alipokuwa akihojiwa na Wakili Peter Kibatala mbele ya Jaji Joackim Tiganga.

Akitoa ushahidi wake, alidai Luteni Dennis Urio bado yuko jeshini na Mbowe alimpa kazi ya kutafuta watu wa kufanya vitendo vya kigaidi.

Pia alidai kuwa hafahamu kama uongozi wa Jeshi la Wananchi Tanzania (JWTZ) ulikuwa unafahamu Luteni Urio anatafuta watu wa kwenda kufanya vitendo vya kigaidi.

SP Jumanne alidai hafahamu kama Mbowe alikwenda nchi mbalimbali kati ya Agosti 2020 mpaka Julai 2021 na kwamba hafahamu kama mamlaka za uchunguzi Tanzania ziliwasiliana na mamlaka za uchunguzi za nje ya nchi.

Wakili Kibatala alihoji akitaka shahidi aseme nani katika timu yao ya upelelezi aliwasiliana na Rais Samia kuhusu kesi hiyo lakini shahidi alidai hafahamu huku akisisitiza kuwa hafahamu kama Mbowe alikimbilia nje ya nchi kukwepa upelelezi kwa sababu alikuwa anajua anashtakiwa kwa ugaidi.Shahidi alidai hawezi kuzungumzia hoja ya kwamba kuna baadhi ya watuhumiwa katika kesi hiyo walifungwa.

Katika maelezo ya onyo ya mshtakiwa wa tatu, Mohammed Ling'wenya, alidai kuwa alieleza kwamba alikwenda Moshi kwa ajili ya kazi ya ulinzi wa kiongozi ambaye ni Mbowe lakini hakuna sehemu inayosema alikwenda kufanya kazi ya ugaidi.

Akiendelea kuhojiwa na Wakili Kibatala, alidai katika maelezo hayo ya onyo hakuna alipokiri kwamba alipewa fedha na Mbowe kwa ajili ya kufanya ugaidi wala hakuna sehemu inayosema Mbowe alipiga simu au kutuma ujumbe wa kumshawishi Ling'wenya kufanya kazi ya ugaidi.

Kibatala alipotaka kujua kama kuna sauti au video ya Mbowe iliyorekodiwa wakati akitoa maelezo kwa Luteni Urio ya kufanya ugaidi, shahidi alidai hakuna sauti wala video ya mshtakiwa huyo.Wakili Kibatala alimhoji shahidi kama anamfahamu Tito Magoti na kuhusika kwake kumteka na shahidi akadai kuwa hamfahamu kabisa Magoti na hajawahi kumteka.

Shahidi alihojiwa anasemaje juu ya taarifa kuwa ni miongoni mwa watu wasiojulikana na ameshiriki kuteka na kutesa watu na kujibu kuwa hajawahi kuteka mtu.

Akiendelea na ushahidi, alidai kuwa katika maelezo ya Ling'wenya, hakuna mahali anapokiri kukutana katika kikao cha kupanga ugaidi na hakuna mahali anakokiri kulipua soko la Kilombero, Arusha.

Pia alidai hakuna sehemu ambayo mshtakiwa Ling'wenya anazungumzia aina ya vilipuzi na kwa uzoefu wake haiwezekani kulipua bila vilipuzi.

Shahidi huyo alidai katika maelezo hayo ya onyo, hakuna mahali Ling'wenya anakiri kuwapo eneo la Rau Madukani kwa ajili ya kupanga ugaidi na hakuna mahali popote alipokiri kwamba walipanga kumdhuru aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya.

Alipotakiwa kusema kama kupigwa risasi Tundu Lissu ni ugaidi au si ugaidi, shahidi huyo alidai ni uhalifu wa kawaida.

"Tufanye ulinganifu, inakuaje kumdhuru mhalifu Sabaya iwe ugaidi lakini kupigwa risasi Lissu isiwe ugaidi?" alihoji Wakili Peter Kibatala na shahidi kujibu kuwa tukio la Mbowe kwa sababu lilikuwa linaendana na kufanya maandamano nchi nzima.

# Muuguzi adaiwa kuuawa kwa mapanga na kuchomwa moto

**Renatha Msungu, DODOMA**

MUUGUZI wa Hospitali ya Taifa ya Magonjwa ya Akili ya Mirembe mkoani Dodoma, Rufina Komba, amefariki dunia baada ya kukatwa mapanga na kuchomwa moto na mume wake katika eneo la Michese jijini Dodoma baada ya kutofautiana na mwenzi wake.

Taarifa kutoka hospitali hiyo inasema Komba huyo alikuwa mfanyakazi wao na msiba uko kwa mama yake mzazi eneo la Miyuji jijini hapa kwa ajili ya taratibu za mazishi.

Akizungumza na Nipashe jana, Dk. Jackson Minja, ambaye ni Katibu wa Afya wa Hospitali, hiyo alisema taarifa ya kifo cha mfanyakazi huyo walizipata juzi na tukio hilo tayari liko mikononi mwa polisi ambao wanaendelea na uchunguzi juu ya mauaji hayo.

Dk. Minja alisema wamesikitishwa na kitendo hicho cha mauaji na hadi sasa hawajui chanzo nini isipokuwa wanasubiri ripoti ya uchunguzi kutoka Jeshi la Polisi ambalo linaendelea kufuatilia.

"Tumeumizwa sana na kifo cha mfanyakazi mwenzetu. Hatuna cha kufanya zaidi ya kusubiri taarifa ya uchunguzi wa polisi," alisema Dk. Minja.

Pia alisema mazishi ya muuguzi huyo yanatarajia kufanyika leo na wafanyakazi wenzake watajumuika na ndugu wa marehemu kwa ajili ya kumhifadhi.

Gazeti hili lilimtafuta Kamanda wa Polisi Mkoa wa Dodoma, Onesmo Lyanga, kutoa ufafanuzi juu ya tukio hilo na kusema yuko nje ya ofisi na kutaka atafutwe msaidizi wake.

Alipotafutwa msaidizi wake alidai kuwa yuko ziarani na kwamba atatoa ufafanuzi juu ya tukio hilo atakaporejea ofisini kwake.

Kutokana na hali hiyo, Nipashe lilifika katika msiba na baadhi ya majirani walisema tukio lililofanywa na mzazi mwenzie marehemu, hivyo kuiomba serikali kufuatilia kwa karibu ili kuhakikisha hatua kali dhidi ya mtuhumiwa zinachukuliwa.

Mmoja wa majirani, Neema Emmanuel, alisema Rufina alikuwa muuguzi mwenye taaluma yake na alikuwa msaada mkubwa katika kusaidia watu kwenye Hospitali ya Mirembe.

Alisema Jeshi la Polisi linapaswa kufuatilia matendo ya kikatili yanayofanywa na wanaume dhidi ya wanawake kila siku ili kukomesha hali hiyo.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233,
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz
Tarehe

Mtaa wa Moshi,
S.L.P. 2888
40470DODOMA,

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya tarehe 12.01.2022 hadi 26.01.2022 kampuni ya MAINLINE CARRIERS LIMTED itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka BANDARI YA DAR ES SALAAM kuelekea JNHPP SITE, gari hilo lenye namba za usajili: T957DTN / T837DJB na T681DUB / T887DJB
2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

| | | |
|---|---|---|
| Urefu | - | mita 20.60 |
| Upana | - | mita 4.50 |
| Kimo | - | mita 4.60 |

3. Njia itakayotumika: BANDARI YA DAR ES SALAAM hadi JNHPP SITE kupitia MKURANGA, KIBITI, MLOKA.

Gari litasafiri muda wa mchana tu (Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.**



KIWANDA CHA UCHAPAJI CHA TAIFA

NPC KIUTA

MIAKA 58 YA MAPINDUZI



Dk. Hussein Ally Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi

**Bodi ya Wakurugenzi, Menejimenti na Wafanyakazi wa Kiwanda cha Uchapaji cha Taifa (KIUTA) tunaungana na Mh. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Hussein Ally Hassan Mwinyi pamoja na Wananchi wote kwa ujumla katika kuadhimisha Miaka 58 ya Mapinduzi matukufu ya Zanzibar.**

**Plot No. 13 Nyerere Road, Postal Address: Box 2320 Dar Es Salaam Tanzania**
**Tel: +255 22 2863216, +255 22 2863418, +255 22 2863209**
**Email: info@npckiuta.co.tz**

# Watoto wafariki dunia wakiwa ndani ya gari kwa kukosa hewa

**Na Maulid Mmbaga**

WATOTO wawili, Abia Joseph (2) na Odilia Msamba (18) ambaye ni dada wa kazi, wamefariki dunia kwa kukosa hewa baada ya kushindwa kufungua milango ya gari lilipojifunga wakati mama yao akiwa kanisani.

Kamanda wa Polisi Kanda Maalumu ya Dar es Salaam, Jumanne Muliro, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo Januari 9, mwaka huu, majira ya saa 7:00 mchana katika mtaa wa Salanga Ungindoni, wilayani Kigamboni.

Muliro alisema wakati tukio linatokea mama wa mtoto huyo, Neema Shayo (33) ambaye ni Mama wa Joseph, alikuwa ibadani kwenye kanisa la Ephata.

Alisema alimwagiza Odilia kwenda kumpa dawa Joseph (mtoto) na baada ya kuingia ndani ya gari lenye namba za usajili T850 DWL, milango ilijifunga na kusababisha kushindwa kutoka.

"Dawa na maji ambazo mtoto huyo alitakiwa kunywa zilikuwa ndani ya gari lililokuwa limeegeshwa nje ya kanisa. Odilia alipewa ufunguo na kwenda kufungua gari hilo akiwa na mtoto baada ya kumaliza kumpa dawa walishindwa kutoka, milango ilijifunga. Walianza kuhangaika na kukosa hewa na kuwa katika hali mbaya.

"Baadaye mama huyo alipobaini dada wa kazi harudi, alikwenda kuangalia pale kwenye gari lake na kuwakuta watoto hao wakiwa kwenye hali mbaya. Jitihada za haraka zilifanyika kuwakimbiza watoto hao hospitalini lakini kwa bahati mbaya wote wawili walipoteza maisha," alisema Muliro.

Aidha, Kamanda Muliro alitoa wito kwa wazazi na walezi na wananchi kwa ujumla kuchukua tahadhari za ziada hasa wanaposhughulika au kuwatuma wasaidizi wa kazi ambao hawajui uwezo na maarifa waliyonayo juu ya mambo wanayowaagiza wafanye.



Katibu Mkuu Msaidizi Idara ya Oganaizesheni ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Taifa, Solomon Itunda (kulia), akimkabidhi Mbunge wa Jimbo la Ilala, Mussa Azzan 'Zungu', fomu ya kuomba kuteuliwa kugombea nafasi ya uspika wa Bunge katika ofisi za makao makuu ya CCM, jijini Dodoma jana. PICHA: IBRAHIM JOSEPH

## Dk. Kijazi apata mrithi TANAPA

**Na Salome Kitomari**

RAIS Samia Suluhu Hassan, amemteua Willium Mwakilema, kuwa Kamishna wa Uhifadhi wa Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA).

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa kwa vyombo vya habari jana, Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu, Jaffar Haniu, uteuzi huo ulianza Januari 8, mwaka huu.

Alisema kabla ya uteuzi huo Mwakilema, alikuwa Naibu Kamishna Uhifadhi wa TANAPA.

"Mhifadhi Mwakilema anachukua nafasi ya Dk. Allan Kijazi ambaye aliteuliwa kuwa Katibu Mkuu, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi," alisema.

Kijazi ameshika nafasi hiyo tangu mwaka 2011 hadi Januari 7, mwaka huu, ikiwa ni mwaka 2011 hadi 2018 akitambulika kama Mkurugenzi Mkuu, mwaka 2018 hadi sasa baada ya Sheria ya Jeshi Usu la Uhifadhi akiitwa Kamishna wa Uhifadhi.

Julai mwaka 2020, aliteuliwa kuwa Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Maliasili na Utalii, mwaka 2021 Rais Samia alimteua kuwa Katibu Mkuu Wizara hiyo huku akiendelea kuwa Kamishna wa Uhifadhi wa TANAPA, hadi juzi alivyoteuliwa kuwa Katibu Mkuu Wizara ya Ardhi.

**Kijazi ameshika nafasi hiyo tangu mwaka 2011 hadi Januari 7, mwaka huu, ikiwa ni mwaka 2011 hadi 2018 akitambulika kama Mkurugenzi Mkuu, mwaka 2018 hadi sasa baada ya Sheria ya Jeshi Usu la Uhifadhi akiitwa Kamishna wa Uhifadh**

# Kinyang'anyiro cha uspika chapamba moto

**Na Paul Mabeja, DODOMA**

KINYANG'ANYIRO cha kugombea nafasi ya Spika wa Bunge kimezidi kupamba moto baada ya wanachama wengine wanane wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), kujitokeza jana kuchukua fomu za kuomba ridhaa ya kuteuliwa.

Kutokana na kujitokeza kwa watu hao jana, sasa idadi ya wana CCM wanaoomba nafasi hiyo wamefikia 17.

Kati ya waliochukua fomu za kugombea nafasi hiyo jana, yumo Sophia Simba, mwenyekiti wa zamani wa Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT) ambaye alikuwa waziri katika serikali ya awamu ya nne chini ya Dk. Jakaya Kikwete.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa katika ofisi za makao makuu ya chama hicho, Katibu Msaidizi Mkuu wa Idara ya Oganaizesheni ya CCM, Solomon Itunda, alisema kazi ya kutoa fomu bado inaendelea na wanachama wenye vigezo wanakaribishwa.

"Kama ambavyo nilisema jana (juzi) uchukuaji fomu unakwenda hadi Januari 15, ambayo ndiyo utakuwa mwisho wa kuchukua fomu ili kutoa nafasi kwa shughuli zingine kuendelea," alisema Itunda.

Alisema wanachama walichukua fomu jana katika kituo cha Dodoma ni pamoja na Mussa Azzan Zungu Mbunge wa Ilala na Mwenyekiti wa Bunge la Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania.

Wengine ni Emmanuel Adamson Mwakasaka, Mbunge wa Tabora Mjini na Mwenyekiti wa Kamati ya Haki, Maadili na Madaraka ya Bunge pamoja na Prof. Handley Mpoki Mafwenga, msimamizi mkuu wa fedha kutoka Wizara ya Fedha na Mipango.

Katika ofisi ndogo ya Lumumba, Dar es Salaam, alisema waliochukua ni Joseph Kasheku Msukuma ambaye ni Mbunge wa Geita Vijijini, Goodluck Ole-Medeve, Sophia Simba, Juma Hamza Chum na Baraka Byabato.

Alisema, ofisi ya Zanzibar kwa siku mbili za kwanza hakuna wanachama hata mmoja ambaye amechukua fomu ya kuomba uteuzi kupitia chama hicho na kutoa wito watu kuzitumia vizuri siku zilizobaki.

Mapema katika ofisi za makao mkuu ya chama hicho, Zungu, akizungumza na waandishi wa habari baada ya kuchukua fomu, alisema ana imani chama chake kitampatia ridhaa ya kukiwakilisha katika kinyang'anyiro hicho.

"Leo (jana) nimekuja kuchukua fomu ya kugombea nafasi hii ya Spika wa Bunge kwa sababu iko wazi, hivyo na mimi kwa mujibu wa maelekezo yalitolewa na chama changu nimeona sifa ninazo hivyo leo nimechukua fomu hii ya kuomba ridhaa ya kuteuliwa na chama," alisema Zungu.

Naye Prof. Mafwenga, alisema toka Bunge lianzishwe, Spika hajawahi kutoka katika utumishi wa umma, hivyo yeye anatamani kuwa wa kwanza.

"Bunge si siasa tu linahitaji mtu ambaye anajua mambo mengi. Mimi hapa nilipo ni mtaalamu wa mambo mengi natoka katika Wizara ya Fedha na Mipango na nina shahada tisa na kama nitakuwa Spika, miswaada ambayo itakuwa haieleweki nipo tayari kuirudisha serikalini hata mara 10," alisema.

# Wafariki kwa kulipukiwa na kitu kinachosadikiwa bomu

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

WATU watatu wamefariki dunia eneo la Msata wilayani Bagamoyo baada ya kulipukiwa na kitu kinachodhaniwa kuwa ni bomu.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Pwani, Wankyo Nyigesa, aliwaambia waandishi wa habari jana kuwa tukio hilo lilitokea juzi majira ya saa 8:00 mchana katika kijiji cha Pongwe Msungura, Kata ya Msata.

Wankyo alisema watu hao waliokota chuma kinachodhaniwa kuwa ni bomu ambacho kililipuka mikononi mwao na kusababisha vifo vyao.

Kwa mujibu wa Kamanda Wankyo, watu hao waliokota kitu hicho kwa lengo la kwenda kukiuza kama chuma chakavu, lakini kiliwalipukia muda mfupi baada ya kukiokota.

Aliwataja waliofariki dunia katika tukio hilo kuwa ni Athumani Ramadhani (20), Maneno Hamis (23) na Abdallah Rajabu (21), wote wakazi wa Msata.

Kamanda Wankyo alitoa angalizo kwa wananchi wanaojihusisha kuuza na kununua vyuma kuwa waangalifu wanapokusanya na vitu vingine kwa lengo la kwenda kuviuza.

Katika tukio lingine, Jeshi la Polisi Mkoa wa Pwani limemfikisha mahakamani Askari wa Jeshi la Wananchi Tanzania (JWTZ), Koplo Chibumba Lugola (35) wa 121 KJ-FIR Sangasanga -Ngerengere Mkoa wa Morogoro kwa tuhuma za mauaji ya mzee wa miaka 62.

Kamanda Wankyo alisema tukio hilo lilitokea juzi majira ya saa 10:00 jioni katika kijiji cha Gumba, kata ya Gwata wilayani Kibaha.

Kwa mujibu wa Wankyo mtuhumiwa anadaiwa kumshambulia Bakari Rashid (62) na kumsababishia kifo akimtuhumu kuhusika na wizi wa kuku bandani kwake.

# Ridhiwani ataka mbinu mpya kumaliza migogoro ya ardhi

**Na Munir Shemweta,** DODOMA

NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Ridhiwani Kikwete, amewataka watendaji wa sekta ya ardhi wanapokwenda kutatua migogoro ya ardhi, wawe na ufumbuzi badala ya kuwa chanzo cha migogoro.

Alitoa kauli hiyo juzi wakati akizungumza na menejimenti ya wizara alipofika kwa mara ya kwanza katika ofisi za wizara hizo zilizoko Mji wa Serikali Mtumba jijini Dodoma baada ya kuapishwa kushika wadhifa huo.

"Haiwezekani nchi hii kuwa na migogoro ya ardhi isiyoisha na kwa bahati nzuri hakuna kitu ambacho hakina sheria. Kila kitu kina sheria zake," alisema Ridhiwani.

Kwa mujibu wa Naibu Waziri huyo, inashangaza kunatokea mgogoro na timu inatumwa kwenda kuutatua lakini timu hiyo inakuwa sehemu ya kuchochea au kuamsha mgogoro jambo alilosema linasababisha kutoeleweka wataalamu hao wanafanya shughuli gani.

Alitolea mfano wa mgogoro wa muda mrefu kati ya vijiji viwili vya Chamakweza na Pingo vilivyoko Chalinze mkoa wa Pwani kuwa ulikuwapo tangu akiwa mdogo na mara kadhaa mawaziri wa wizara hiyo kwenda kushughulikia lakini ufumbuzi wa mgogoro huo haujapatikana.

"Mgogoro wa vijiji hivi ulikuwapo tangu nikiwa mdogo. Ameshakuja waziri akiwa (William) Lukuvi, waziri akiwa (John) Chiligati. Kila unayemjua katika wizara hii amekwenda lakini kwa nini hauishi? Ninyi kama wataalamu lazima mtuletee jibu.

"Sisi tunataka twende na solution (suluhisho) siyo tukasimuliwe alikuja fulani na tukaingizwa kwenye orodha ya watu walioenda halafu hakuna matokeo. Sasa kama wataalamu ni lazima tuje na solution (suluhisho)," alisema.

Pia aliwataka wataalamu wa wizara na taasisi zake kuangalia namna ya kuchangia uchumi wa nchi na kubuni miradi inayoweza kuingizia serikali fedha.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Allan Kijazi, alihimiza ushirikiano kwa ngazi zote za wizara na kubainisha kuwa mara nyingi majukumu yanakwama kutokana na chokochoko na uzembe wa baadhi ya watendaji.

Alisema hali hiyo husababisha kukwama kwa kazi na kusisitiza kwamba hatavumilia uzembe utakaokwamisha utekelezaji malengo waliyokabidhiwa na taifa.

Kwa mujibu wa Kijazi Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ni nyeti na karibu kila mtu anaguswa nayo na chohote kitakachofanyika kinyume cha maelekezo au matarajio, kitasababisha kelele.

"Wizara hii ni nyeti na karibu kila mtu anaguswa nayo na kelele zinachafua taswira ya wizara na nchi pamoja na Rais aliye madarakani maana ametutuma kusimamia," alisema Kijazi.


SHIRIKA LA BIMA ZANZIBAR

MIAKA 58 YA MAPINDUZI



Dk. Hussein Ally Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi

**Bodi ya Wakurugenzi, Menejimenti na Wafanyakazi wa Shirika la Bima la Zanzibar tunaungana na Mh. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Hussein Ally Hassan Mwinyi pamoja na Wananchi wote kwa ujumla katika kuadhimisha Miaka 58 ya Mapinduzi matukufu ya Zanzibar.**

COASTAL ZONE (DAR ES SALAAM)
Lumumba/ Morogoro Road, Opp. Vijana Building Plot No 65 P.O.Box 8631, Dar es Salaam Tel: Direct +255 22 2182639 Fax: +255 22 2183161 Email: HYPERLINK "mailto:zicdsm@zic.co.tz" \t "_blank" zicdsm@zic.co.tz

HEAD OFFICE
Maisara/ Mpirani P. O. Box 432, Zanzibar Tel: +255 24 2232676/2233867/2239504 Fax: +255 24 2232422 Email: HYPERLINK "mailto:zichq@zic.co.tz" \t "_blank" zichq@zic.co.tz

LAKE ZONE(MWANZA)
Alpha Building, 2nd Floor P. O. Box 829, Mwanza Tel: +255 28 2500168 Fax: + 255 28 2500410 Email: HYPERLINK "mailto:zicmwa@zic.co.tz" \t "_blank" zicmwa@zic.co.tz

NORTH ZONE (ARUSHA)
Mtaa wa Sokoine P. O. Box 13088, Arusha Tel: +255 27 2547314 Fax: +255 27 2547422 Email: HYPERLINK "mailto:zicar@zic.co.tz" \t "_blank" zicar@zic.co.tz

SOUTHERN ZONE (MBEYA)
P. O. Box 6296, MBEYA Tel: +255 250 250 3681 Fax : +255 250 250 3684 Email: HYPERLINK "mailto:zicmby@zic.co.tz" \t "_blank" zicmby@zic.co.tz

PEMBA OFFICE (CHAKE CHAKE)
P. O. Box 324,Wete - Pemba Tel/Fax +255 24 2452151 Email: HYPERLINK "mailto:zicpba@zic.co.tz" \t "_blank" zicpba@zic.co.tz

CENTRAL ZONE (DODOMA)
P. O. Box 4488 Tel: +255 26 2320063 Fax: +255 26 2320064

MTWARA OFFICE (MTWARA)
Market Street (Sokoni), Kikongola Road, Bus Stand Tel: +255 23 2333100 Fax: +255 23 2333131

KAHAMA SALES OFFICE
P.O.Box 829, Posta BuildinIsaka Road Kahama - Shinyanga

TANGA SALES OFFICE
P.o.box13088 Posta Building Independence Street Tanga

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Magari ya serikali yadhibitiwe ajali barabarani

**WAANDISHI** sita na wananchi wengine wanane wamefariki dunia jana kwenye ajali ya gari iliyotokea eneo la Nyashomi wilayani Busega, mkoani Mwanza wakiwa kwenye msafara wa Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, kuelekea Ukerewe.

Ajali hiyo imetokana na gari yenye namba za usajili STK 8140 iliyokuwa imebeba waandishi ambayo ilikuwa kwenye mwendokasi baada ya kulikwepa basi la Batiko lilitokea Musoma kuelekea Mwanza kugongana uso kwa uso na Hiace.

Ajali hii inatokea huku waandishi wanne mkoani Mtwara, wakiendelea kuuguza majeraha ya ajali waliyoipata wakiwa kwenye ziara ya Mkuu wa Mkoa huo Desemba 2, mwaka jana.

Nyingine ni wafanyakazi sita wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), waliofariki kwa ajali wilayani Mbarali, mkoani Mbeya.

Hizi ni chache kati ya nyingi zilizohusisha magari ya serikali na mashirika ya umma.

Mathalani, kwa Dar es Salaam ni kawaida kuona gari lenye namba za serikali au ubalozi kupita njia tofauti na anayotakiwa kupita kwa kisingizio cha kuwahi anakokwenda.

Madereva wa magari hayo huwasha taa na kupiga ving'ora au honi na kuwaweka kwenye wakati mgumu madereva wengine wanaojaribu kuwapisha kwenye njia yenye msongamano wa magari.

Chakushangaza maofisa wa serikali waliomo ndani ya magari hayo wanashuhudia madereva wao wanavyovunja sheria za barabarani, lakini hawawakemei wanachojali ni kufika wanakoelekea.

Madereva hao huendesha kwa mwendokasi na kama giza limeshaingia wanawasha mwanga mkali wa taa kwa dereva aliye mbele yake kuashiria aongeze mwendo bila kujali mbele kuna magari mengine, hali ya barabara au alama za usalama barabarani.

Mfano ajali ya Simiyu, Kamanda wa Polisi mkoani humo, amethibitisha chanzo ni mwendokasi wa gari ya serikali ambayo ilikuwa inakwepa basi na kuishia kugongana uso kwa uso na Hiace, kwa kugharimu maisha ya watu 14 na wengine kujeruhiwa.

Ni muhimu sasa polisi wa usalama barabarani wakapewa rungu la kutoza faini magari ya serikali bila kujali ni la kiongozi gani ili kuokoa maisha ya wanaobebwa kwenye magari hayo. Madereva wa serikali wanajiona wako juu ya sheria wanaweza kufanya lolote wakati wowote.

Ni lazima kupinga hali hii kama kuna foleni wasubiri au watumie mtandao wao kuwasiliana na askari wanaoongoza magari kwenye eneo fulani wavute magari kwa wingi hadi afikiwe kuliko kulazimisha kupita katikati ya barabara yenye msongamano wa magari.


Mathalani, barabara kama ya Tabata au eneo la Lugalo Dar es Salaam ni ngumu magari matatu kupita kwa pamoja, maana yake wapo ambao watakaribia kutumbukia kwenye mtaro wakati wanawapisha wanaotanua.

Wakati mwingine ni baadhi ya magari ya vyombo vya ulinzi na usalama ambayo bila kujali huwasha taa, kupiga honi na kulazimisha kupita kusikostahili kwa mujibu wa sheria za usalama barabarani.

Kwa ujumla madereva hasa wanaoendesha viongozi hujiona wako juu ya sheria na wakati mwingine kusababisha ajali ambazo zinaweza kuepukika.

Tunakumbuka ajali iliyotokea mwishoni mwa mwaka jana, mkoani Tanga kwa mabasi mawili ya chombo kimoja cha ulinzi na usalama kulazimisha kupita magari mengine na kusababisha magari zaidi ya 10 kugongana huku baadhi ya watu kujeruhiwa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Mapinduzi yaendelee kuwa nguzo ya umoja wa Zanzibar

**LEO** ni kilele cha maadhimisho ya miaka 58 ya Mapinduzi ya kumng'oa sultan na kuifanya Zanzibar kuwa huru na baadaye kuungana na Tanganyika na kuzaliwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mapinduzi hayo ya mwaka 1964 yamepitia miongo mingi, taifa likipanda milima na kushuka mabonde hadi kusimama na kuwa na watu wenye umoja na kuheshimiana bila kujali itikadi za kisiasa. Wazanzibari wameendeleza umoja kutokana na ukweli kwamba, umoja katika jamii au taifa, ni jambo muhimu kutokana na ukweli kwamba ndiyo nguzo ya maendeleo.

Mapinduzi ya Zanzibar yamefanikisha kupiga hatua mbalimbali za maendeleo na hasa kuimarisha umoja wa watu wake, ni wazi kwamba wakiendelea kuusimamia umoja huo watafika mbali kimaendeleo.

Mwaka 1964 Zanzibar ilifanya mapinduzi ya kumwondoa sultan Jamshid bin Abdullah na kuondoa kila aina ya ubaguzi uliokuwapo enzi hizo na kuendeleza umoja na kuuimarisha zaidi huku ikijenga jamii huru na yenye kujitambua.

Uunganishaji wa wananchi wa Zanzibar kwa kuwa na Serikali ya Umoja wa Kitaifa (SUK), kwa ajili ya kuimarisha udugu wao uliotishia kusambaratika kutokana na itikadi za kisiasa, ni miongoni mwa mambo ya kujivunia katika kuenzi Mapinduzi.

Mafanikio hayo ya kuwaunganisha Wazanzibari ni hatua ambayo kila mmoja angependa iwe endelevu na kuungwa mkono na watu wote kuanzia viongozi wa serikali, dini na wananchi.

Hata Rais wa sasa wa Zanzibar Dk. Hussein Ali Mwinyi amekuwa akisisitiza umuhimu wa kuimarisha umoja kwa lengo la kuleta maendeleo, jambo ambalo kimsingi linaongeza amani na utulivu.

Wazanzibari wanapoadhimisha miaka 58 ya Mapinduzi ni vyema waendelee kuimarisha umoja huo, kwa kuwa ni wamoja bila kubaguana kwa itikadi za kisiasa ambazo miaka ya nyuma zilitaka kuchukua nafasi kubwa.

Hatua ya kuwapo Serikali ya Umoja wa Kitaifa ni dalili kwamba, Wazanzibari wameamua kuungana na kuwa wamoja, hivyo jambo la msingi ni kuendelea kutambua kuwa itikadi za kisiasa hazina nafasi ya kuwafanya wabaguane.

Kwa kuwa Wazanzibari wamefanikiwa kuwa na umoja huo, ni wazi kwamba wataendelea kufanya kazi na kujiletea maendeleo hasa wakati huu ambao serikali ina mkakati kuimarisha uchumi wa buluu.

Uchumi wa buluu unatafsiriwa kuwa ni shughuli za kiuchumi zinazohusu matumizi bora ya rasilimali za bahari, ili kuimarisha au kukuza uchumi kuanzia sekta ya uvuvi inayoelezwa kuchangia asilimia 2.6 ya pato ghafi la Zanzibar.

Lakini, pia ni muhimu kwa kuwa inatoa ajira za moja kwa moja kwa watu 200,000, wakati zaidi ya wengine 100,000 hutegemea sekta hiyo na kwamba, kuna nafasi kubwa ya kuifanya Zanzibar na Tanzania kwa ujumla kuwa na uchumi bora zaidi kwa kufanyia maarifa zaidi uchumi wa buluu.

Hivyo wakati serikali ikiwa kwenye mikakati hiyo, jambo la muhimu ni Wazanzibari wenyewe kuendelea kuimarisha umoja wao ambao pia umechangia kuwapo kwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa.

Katika baadhi ya hotuba zake, Rais Mwinyi amekuwa akirudia mara kwa mara kwamba, anaheshimu maridhiano na matakwa ya kikatiba ya kushirikiana na vyama vingine vya siasa katika kuendesha serikali.

Anasema, yuko tayari kutekeleza maridhiano kama katiba ya Zanzibar inavyotaka, kuyaendeleza na kuyastawisha, na kwamba ni wajibu wa viongozi wa vyama vya siasa, wananchi na jamii kushiriki katika kuimarisha umoja huo.

Akiwa kiongozi wa taifa, anaahidi kujitahidi kwa kadri ya uwezo wake kuyajenga na kuyadumisha maridhiano kwa maslahi ya Zanzibar na kwamba, yaliyo ndani ya mamlaka kwa uwezo wake atayatekeleza bila hofu.

**TANGAZO**

# MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA

**Imethibitishwa na ISO 9001: 2015**

# SALAMU ZA PONGEZI

Bodi ya Wakurugenzi, Menejimenti na Watumishi wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), tunatoa pongezi za dhati kwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, **Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi** kwa kuadhimisha **Miaka 58 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar.**

## MAPINDUZI DAIMA!

**Mungu Ibariki Tanzania**

**Mungu Ibariki Afrika**



**Hayati Sheikh Abeid Amani Karume**
**Rais wa Awamu ya Kwanza wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi**



**Hayati Aboud Jumbe Mwinyi**
**Rais wa Awamu ya Pili wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi**



**Mhe. Ali Hassan Mwinyi**
**Rais wa Awamu ya Tatu wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi**



**Hayati Idris Abdulwakil Nombe**
**Rais wa Awamu ya Nne wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi**



**Mhe. Dkt. Salmin Amour Juma**
**Rais wa Awamu ya Tano wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi**



**Mhe. Amani Abeid Karume**
**Rais wa Awamu ya Sita wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi**



**Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein**
**Rais wa Awamu ya Saba wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi**



**Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi**
**Rais wa Awamu ya nane wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi**

***"Pamoja Tunajenga Taifa Letu"***

# Mkemia ataka wasafirisha kemikali kusajiliwa

**Na Mary Geofrey**

MKEMIA Mkuu wa Serikali, Dk. Fidelice Mafumiko, amewataka wasafirishaji wa kemikali nchini, kusajiliwa na Msajili, kutoa taarifa ya mzigo unaosafirishwa kwa kuzingatia mahitaji yanayotakiwa wakati wa usafirishaji wa kemikali husika.

Alisema pia kila msafirishaji anapaswa kuzingatia aina ya gari linalohitajika kwa ajili ya kubeba mzigo wa kemikali husika na kuwa na kibali cha usafirishaji wa kemikali husika.

Dk. Mafumiko alitoa wito huo, jana jijini Dar es Salaam, wakati akifungua kikao cha wadau wanaosafirisha kemikali hatarishi nchini, katika kujadili namna ya kuboresha utekelezaji wa Sheria ya Kemikali katika usafirishaji na usalama wake.

Alisema Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA), inatekeleza Sheria ya Usimamizi na Udhibiti wa Kemikali za Viwandani na Majumbani Na. 3 ya mwaka 2003, na 2 Kanuni zake za mwaka 2020.

"Kutokana na uzoefu uliopo sasa katika kusimamia usafirishaji wa kemikali, mamlaka imeweza kubaini changamoto mbalimbali.

Baadhi ya changamoto hizo ni madereva kusafirisha kemikali bila kuwa na mafunzo ya usafirishaji salama wa kemikali, upakiaji na upakuaji wa mizigo ya kemikali hatarishi na ambazo zilishatolewa maelekezo ya usimamizi wake kufanyika pasipo kuwapo na wakaguzi," alisema Mafumiko.

Alieleza kuwa wamebaini, wasafirishaji kutokuwa na vibali vya usafirishaji, mizigo ya kemikali kuchanganywa na vitu vingine kama vile chakula na mkaa, ukosefu wa sehemu maalumu za kuegesha magari yaliyobeba kemikali na ubovu wa baadhi ya magari yanayotumika kusafirisha kemikali kama sheria inavyoelekeza.

Dk. Mafumiko alisema katika kukabiliana na changamoto hizo, mamlaka imekuwa ikifanya jitihada mbalimbali, ikiwa ni sehemu ya kuzitatua wakati wa usafirishaji wa kemikali hatarishi.

Alitaja jitihada hizo ni kutoa mafunzo kwa madereva juu ya usafirishaji salama wa kemikali, kuandaa miongozo ya usafirishaji wa kemikali hatarishi na kushirikiana na wadua mbalimbali katika kutatua changamoto ambazo ziko nje ya majukumu ya mamlaka.

Naye Mtendaji Mkuu wa Chama cha Wasafirishaji Tanzania (TAT), Hussen Wandwi, alisema wasafirishaji wanatakiwa kufuata taratibu zote kabla ya kuanza kusafirisha mzigo wa aina yoyote.

Alisema wanakabiliwa na changamoto ya uhaba wa elimu kwa madereva na wananchi wanaowakuta njiani wakati wakisafirisha kemikali.




Bango likiwa limeanguka na kuzuia njia ya waenda kwa miguu katika barabara ya viwandani, Mikocheni mkoani Dar es Salaam jana. PICHA: SABATO KASIKA

## Watalii wamiminika Kisiwa cha Nungwi

**Na Steven William,** ZANZIBAR

WATALII kutoka nje wameanza kumiminika katika vivutio vya utalii vilivyoko Nungwi, visiwani Zanzibar.

Watalii hao wameanza kumiminika kuanzia mwaka mpya huku wawekezaji wa vivutio hivyo wakifurahia neema hiyo.

Kundi hilo la watalii kutoka ndani na nje lilianza kuingia Zanzibar baada ya serikali ya Rais Dk. Hussein Mwinyi kufungua mipaka yake ambayo ilikuwa imefungwa kutokana na janga la corona.

Mwongoza watalii katika Kisiwa cha Nungwi, ambaye hakutaka kutaja jina lake, alisema mpaka sasa wanapokea wageni mbalimbali kutoka nje na ndani kwa ajili ya kufanya utalii.

Alisema kutokana na janga la corona kupungua na mipaka kufunguliwa, sasa watalii wameanza kuingia nchini hususani katika vivutio vya utalii Nungwi nje kidogo na mji wa Unguja.

Alisema katika mradi wa kupokea watalii, vijana wamepata ajira na pia wananchi watapata fursa ya kufanya biashara kwa watalii wanaofika sehemu hiyo.

Juma Selema Hassan, mkazi wa Nungwi, alisema watalii wanaofika katika mji wa Nungwi wanaingiza fedha za utalii serikalini.

Mfanyabiashara katika eneo la Nungwi visiwani Zanzibar Suleiman Hassan, alisema anawakaribisha wawekezaji wakubwa na wadogo kwa kuwa milango iko wazi ili vijana wapate ajira.

Alisema sasa wakati umefika wananchi kuwapeleka watalii hao kwa mikono miwili kwa kuwa kuna vivutio vingi.

# Jafo ahimiza Watanzania kupanda miti

**Na Joseph Mwendapole**

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Dk. Selemani Jafo, amewataka Watanzania wapande miti kwa wingi kwa ajili ya kulinda mazingira ili kuepuka joto linalosababishwa na mabadiliko ya tabianchi.

Aliyasema hayo jana katika ziara yake ya siku moja kwenye msitu wa Kazimzumbwi ulioko Pugu Mkoa wa Pwani akiambatana na viongozi wa Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira (NEMC).

Jafo alipongeza Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS), kwa namna wanavyotunza misitu ya Tanzania ukiwamo wa Kazimzumbwi na kuifanya iwe kivutio kwa watalii.

"Nimefarijika sana kufika hapa na kuona namna msitu huu wa Kazimzumbwi unavyotunzwa. Nafahamu Mtendaji Mkuu TFS hayupo hapa lakini wahusika mfikishieni salamu za pongezi kwani amefanya kazi kubwa sana ya kusimamia misitu yetu na sasa imekuwa na manufaa makubwa kwa utalii wa nchi yetu," alisema Jafo.

Alisema utunzaji mzuri wa misitu hiyo umesababisha ongezeko kubwa la watalii kutoka 533 mwaka 2017 hadi 10,206 mwaka jana huku idadi ya wazawa wanaofika hapo ikiwa kubwa zaidi kulinganisha na wageni.

Waziri Jafo aliwataka wananchi wanaookaa jirani na misitu waache kuchoma miti ovyo kwa kuwa misitu hiyo ndiyo imekuwa ikisaidia kupunguza joto wakati wa mabadiliko ya tabianchi ambayo yamekuwa yakisababisha ongezeko la joto.

"Niwaombe Watanzania wote sasa tuwekeze kwenye utunzaji wa mazingira kwani hali ya sasa kiwango cha joto kimeongezeka sana na kila halmashauri ipande miti milioni 1.5," alisema

"Najua hali ya upandaji wa miti ilisuasua kutokana na ukame wa muda mrefu lakini kwa sababu mvua zimeanza kunyesha kazi hiyo iendelee na kila halmashauri itumie mvua hizo kupanda miti na wakuu wa wilaya na mikoa wasimamie," alisema

Pia Waziri Jafo alisema anafahamu kila halmashauri imepewa mwongozo wa kusimamia vitalu kwa lengo la kusaidia kwenye maeneo mbalimbali kama shule na taasisi zingine.

"Huko duniani tumejisifu kwamba sisi tumehifadhi ekari milioni 48.1, hivyo Watanzania tuendelee na ajenda yetu hii ya kutunza na kulinda mazingira yetu kwa kuhakikisha tunapanda miti mingi zaidi," alisema Jafo

Naye Mkurugenzi Mkuu wa NEMC, Dk. Samuel Gwamaka, alimpongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuweka kipaumbele kwenye utunzaji na uhifadhi wa mazingira jambo ambalo limesaidia kuweka chachu.

Alisema mazingira ya Kazimzumbwi Pugu yametunzwa vizuri na yamekuwa kivutio kikubwa kwa watalii wa ndani na nje ya nchi kutokana na mazingira kuwa safi na ya kuvutia.

Dk. Gwamaka alisema kila familia inapaswa kupanda miti angalau mitatu ili iweze kusaidia kupunguza hali ya joto panapotokea mabadiliko ya tabianchi na kwamba maisha bora yatapatikana tu pale mazingira yatakapokuwa yameboreshwa na kulindwa.

## Maofisa kilimo wapatiwa pikipiki kuelimisha kilimo cha pamba

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

SERIKALI wilayani Kahama imesema, itawachukulia hatua za kisheria maofisa kilimo wa kata katika Halmashauri ya Msalala, watakaobainika kutotimiza majukumu yao ya kwenda vijijini kutoa elimu ya kilimo cha pamba, kwa kuwa wamepatiwa vyombo vya usafiri.

Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Festo Kiswaga, alitoa kauli hiyo jana katika hafla maalumu ya makabidhiano ya pikipiki tatu zenye thamani ya Sh. milioni 6.3 zilizotolewa na Bodi ya Pamba Tanzania kwa maofisa kilimo wa halmashauri hiyo.

Kiswaga alisema, pikipiki hizo ni lazima zilete matokeo chanya kwa kuhakikisha wakulima wa zao la pamba wanapatiwa elimu ya kilimo cha kisasa ikiwa ni pamoja na kupatiwa mbolea na dawa za kudhibiti wadudu kwa wakati ili wazalishe kwa tija.

"Sisi serikali tutawapima kwa utendaji kazi wetu, msikae ofisini nendeni mkawahudumie wakulima wetu, pikipiki hizi zitumike kwenye shughuli za kilimo pekee, zitunzeni ili ziwasaidie wakulima hususani wa vijijini ambao wanahitaji msaada wenu," alisema Kiswaga.

Naye Mkurugenzi wa halmashauri hiyo, Charles Fussi, alisema katika mwaka wa fedha 2021/22, halmashauri inatarajia kununua pikipiki saba kwa ajili ya maofisa kilimo wa kata ili kuwawezesha kutimiza majukumu yao hususani ya kuwahudumia wakulima kwa kuwafuata shambani.

Alisema, halmashauri ina upungufu wa pikipiki 38 kwa maofisa kilimo ngazi za kata, zilizopo ni pikipiki 19 pekee na jana wamepokea tatu na kufikia idadi ya 22 ambazo zilitolewa kwa maofisa ugani wa kata za Bugarama, Lunguya na Ikinda.

Kwa upande wake Ofisa Kilimo wa halmashauri hiyo, Zedekia Solomoni, alisema wakulima wa halmashauri hiyo kutoka kata 18 wamelima ekari 2,576 za zao la pamba katika msimu wa kilimo 2021/22 na wanatarajia kuvuna kilo milioni 1.5.

Pia Ofisa Kilimo Mkuu wa Bodi ya Pamba wilayani hapo, Emmanuel Kileo, alisema wataendelea kutoa pikipiki kwa maofisa kilimo ngazi ya kata katika halmashauri za Ushetu, Msalala na Manispaa ya Kahama, lengo likiwa kuinua kilimo cha pamba na kuongeza kipato cha mkulima.

"Kadiri bajeti yetu itakavyokuwa inaimarika kila mwaka tutaendelea kununua vyombo vya usafiri (pikipiki) na kuwapatia maofisa kilimo wetu ili kuhakikisha Kahama inaongoza katika uzalishaji wa pamba safi na zisizokuwa na maji na mchanga," alisema Kileo.

# Walimu kusajili wanafunzi darasa la kwanza saa 24

**Na Neema Hussein,** KATAVI

MKUU wa Mkoa wa Katavi, Mwanamvua Mrindoko, amewataka walimu kuwapo shuleni saa 24 kwa ajili ya kupokea wanafunzi wanaoandikishwa kuanza darasa la kwanza na awali ili mzazi akifika asirudi na mtoto nyumbani kwa kukosa huduma.

Mrindoko aliyasema hayo jana baada ya kukabidhiwa madarasa 87 yaliyojengwa kwa fedha ya UVIKO-19 katika Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo, mkoani Katavi.

Mrindoko alisema kila siku ifikapo saa 12 jioni ni lazima apate taarifa ya uandikishaji katika ofisi yake ili aweze kujua kama kuna kuongezeka au kupungua kwa idadi ya uandikishaji pia kujua nani kafanya vizuri na aliyefanya vibaya.

"Hii ni wiki ya kazi na sio wiki ya kupumzika, mzazi akija ametoka shamba amechelewa hata kama ni saa mbili usiku ni lazima ahudumiwe ili tuhakikishe hakuna mzazi au mlezi anayerudishwa nyumbani," alisema Mrindoko.

Hata hivyo, aliwataka viongozi wa dini, kimila na mitaa kuwahimiza wazazi wenye watoto waliofikisha umri wa kusajiliwa kuanza shule wanawafikisha na kuwaandikisha.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Nsimbo, Mohamed Ramadhan, matarajio yao yalikuwa ni kusajili watoto 5,596 kwa darasa la kwanza, lakini mpaka Ijumaa wiki iliyopita walisajili watoto 1, 666 sawa na asilimia 29.7.

Ramadhan alisema kwa upande wa awali matarajio yao yalikuwa ni kusajili watoto 4, 834, lakini mpaka Ijumaa walikuwa wamesajili watoto 755 sawa na asilimia 14.

Alisema moja ya jitihada zilizofanyika ni kuhakikisha walimu wote wanakuwapo shuleni kuanzia Januari 10 kwa ajili ya kusajili watoto na ofisi zote za walimu zitakuwa wazi.



Kada wa CCM Ambwene Kajula akirudisha fomu ya kugombea uspika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mjema aonya uharibifu alama za barabarani

**Na Marco Maduhu,** KISHAPU

MKUU wa Mkoa wa Shinyanga Sophia Mjema, ameonya tabia ya baadhi ya wananchi mkoani humo, kuharibu alama za usalama barabarani.

Mjema alitoa onyo hilo jana wakati akikagua ujenzi wa miundombinu ya barabara na madaraja wilayani Kishapu.

Alisema alama za usalama barabarani ni muhimu katika kuzuia ajali na baadhi ya wananchi wana tabia ya kuzing'oa alama hizo.

"Naombeni wananchi muitunze miundombinu ya barabara na madaraja haya, ili idumu kwa muda mrefu kuwahudumia na kufanya shughuli zenu za kiuchumi bila ya kupata vikwazo na msing'oe alama za usalama barabarani kwa ajili ya usalama wenu," alisema Mjema.

Aliwaagiza Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) mkoani humo, kudhibiti magari yenye uzito mkubwa kutopita kwenye barabara na madaraja ili kutoharibu miundombinu hiyo na kuingiza hasara serikali ya kutenga fedha za marekebisho ya mara kwa mara.

Katika hatua nyingine, aliwataka makandarasi ambao wanatekeleza miradi hiyo ya ujenzi wa miundombinu ya barabara na madaraja, waitekeleze kwa ubora unaotakiwa na kuhudumia wananchi kwa muda mrefu.

Kwa upande wake, Kaimu Meneja wa TANROADS mkoani Shinyanga, Mhandisi Jessica Manang, alisema magari yanayoruhusiwa kupita kwenye barabara na madaraja hayo yasizidi tani 50, huku akiahidi kulifanyia kazi agizo hilo la kudhibiti magari yenye uzito mkubwa kupita kwenye miundombinu hiyo.

Naye Diwani wa Ukenyenge, Anderson Mandia, alisema ujenzi wa daraja kubwa katika eneo hilo lenye thamani ya Sh. bilioni 1.5, litakuwa msaada mkubwa kwa wananchi, ambao wataepukana na ajali, pamoja na kulitumia kufanya shughuli zao za kiuchumi.

Nao baadhi ya wananchi wa Kishapu kwa nyakati tofauti walisema, ujenzi wa miundombinu hiyo ya Ukenyenge na Itilima, utawasaidia katika shughuli zao za kiuchumi, hasa wakati wa kusafirisha mazao na kuahidi kushirikiana na serikali kuilinda.

# Wanafunzi wapata mkombozi wa manyanyaso ya daladala

**Na Sabato Kasika**

CHAMA cha Kutetea Abiria nchini (CHAKUA), kimeanzisha idara ya huduma kwa wanafunzi na watoto, itakayokuwa na jukumu la kuhakikisha wanasafiri katika daladala bila usumbufu, kwenda shule na kurudi nyumbani.

Akizungumza na gazeti hili, jijini Dar es Salaam jana, Mwenyekiti wa chama hicho, Hassan Mchanjama alisema, CHAKUA inatetea abiria wote, imeanzisha idara hiyo kutokana na manyanyaso wanayopata.

"Baadhi ya makondakta na madereva wa daladala ni kero kwa wanafunzi, hivyo tumeona tuwe na idara ambayo itasaidia kupunguza kero hizo ili watoto wetu wanapokwenda shule wasisumbuliwe," alisema Mchanjama.

Mwenyekiti alimtaja Adinan Mbezi kuwa ndiye aliyepewa jukumu la kuongoza idara hiyo ili kuhakikisha abiria hasa wanafunzi na watoto wanapata huduma ya usafiri bila usumbufu.

"CHAKUA inatetea na kuelimisha abiria wote wakiwamo wanafunzi na watoto, hivyo kuanzishwa kwa idara hii, tafsiri yake ni kwamba, wanafunzi wametengewa idara yao, ili wasiendelee kunyanyasika," alisema.

Mkuu wa idara hiyo, Adinan Mbezi, alisema idara hiyo itaanza kazi wiki ijayo kwa kukutana na wadau wote wa usafirishaji, wakiwamo wamiliki wa vyombo vya usafiri, vyama vya madereva, makondakta na wengine.

"Jumatatu ijayo tutatoa semina ili kuwaelimisha kuhusu umuhimu wa kuwachukua wanafunzi kwa ajili ya kuwahi shule na tunaamini kwamba katika semina hiyo, kila mmoja atatoa dukuduku lake," alisema Mbezi.

Alisema, baada ya semina hiyo, kitakachofuata na wafanyakazi wa idara hiyo kwenda kwenye vituo vya daladala kuona kama madereva na makondakta wanazingatia elimu watakayokuwa wamepewa.

"Tunataka kuanzia jijini Dar es Salaam hasa kwenye vitu sugu kama Gongo la Mboto, Mbezi Mwisho kwenda Makabe au Mpiji Magoe, ambako wanafunzi wananyanyasika, kisha tutakwenda mikoani," alisema.

Mbezi alifafanua kuwa, watafanya kazi hiyo kwa kushirikiana na askari wa usalama barabarani, ili kusaidia wanafunzi kuondokana na kero hiyo ambayo bado haijapatiwa ufumbuzi wa kudumu.

"Eneo lingine ambalo tutashughulika nalo ni kwenye shule binafsi na za serikali zinazotoa huduma ya usafiri wa wanafunzi, kwa kuwa huko pia kuna tatizo kubwa linalohitaji kufanyiwa kazi haraka," alisema.

Alisema, baadhi ya mabasi ya shule hizo hujazana wanafunzi kupita kiasi na wengine kupakatana, na kufafanua kuwa mazingira kama hayo si salama kwao na kwamba idara hiyo itafuatilia kwa karibu kero hiyo.

Mbezi alisema, siku yoyote idara yake itasambaza waraka wa serikali katika shule hizo, ambao unahusu kumsafirisha mwanafunzi akiwa salama aendapo shuleni na arudi nyumbani.

"Sisi kama wadau wa usafiri tumeona tushirikiane na serikali katika mambo hayo kwa ajili ya usalama wa watoto wetu na kama wahusika watakaidi, itabidi vyombo vya dola viwashurutishe," alisema.

Alisema, mtindo wa kujaza wanafunzi katika basi una madhara mengi yakiwamo ya kusababisha ajali au kuambukizana ugonjwa UVIKO-19 na kwamba wao kama wadau hawataki hilo litokee.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Seleman Jafo (kulia), akikagua mazingira katika Msitu wa Pugu Kazimzumbwi, jijini Dar es Salaam jana. Wengine ni maofisa wa Wakala wa Misitu (TFS) na Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC). **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Grosso Foods waja na mikakati mipya kuboresha kilimo Tanzania

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Uwekezaji katika Sekta ya Kilimo nchini, Grosso Foods B.V imebadili jina, sasa inafahamika kama Grosso.Africa, ikibainisha mipango yake mipya ya kuleta mageuzi makubwa ndani ya Sekta ya Kilimo nchini kwa kuwawezesha wakulima kuongeza mavuno yao na kuwa na uhakika wa masoko baada ya mavuno.

Pamoja na shughuli zingine, Grosso. Africa ni wasambazaji na wakodishaji wa nyenzo za kilimo ikiwamo matrekta aina ya LS na bidhaa zingine za kilimo za JAN na mbegu bora za mazao ya biashara.

Grosso.Africa ni watoaji wa elimu kuhusu kilimo cha kisasa kwa wadau wa Sekta ya Kilimo wakiwamo wakulima wadogo na wakubwa kupitia wataalamu wake ambao ni wabobezi wa masuala ya kilimo duniani lengo likiwa ni kuwawezesha wakulima hao kufanya kilimo cha kisasa na kuongeza mavuno na hatimaye kunufaika na shughuli za kilimo.

Taarifa iliyotolewa kwa vyombo vya habari na uongozi wa kampuni hiyo jana, ilisema Gross.Africa inatambua ardhi ni mali muhimu kwa mkulima wa Kiafrika, hivyo imejizatiti kuboresha ardhi kwa kuifanya kuwa yenye rutuba na kutatua vikwazo vinavyowakabili wakulima ikiwamo ukosefu wa mbegu bora.

Pia, mabadiliko yaliyofanyika ndani ya kampuni yamehusisha maboresho ya tovuti kwa lengo la kuboresha zaidi utoaji wa taarifa kuhusu kilimo cha kisasa na taarifa zingine kwa wadau wa biashara na uwekezaji wa Sekta ya Kilimo nchini na Afrika kwa ujumla.

"Jina letu jipya linaelezea mwelekeo mpya wa kampuni, pia linaonyesha ni kwa namna gani tumejizatiti kushirikiana na wadau wetu ambao wametusaidia kufika hapa tulipo.

"Pia mabadiliko yanalenga kudumisha uhusiano wetu na wadau kwa miaka mingi ijayo," alisema Nuradin Osman, Mwanzilishi na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Grosso. Africa.

Aliongeza: "Mkataba wetu mpya wa usambazaji wa nyenzo bora na za kisasa za kilimo ikiwamo matrekta ya LS na bidhaa za JAN unaashiria utayari wetu na namna gani tumejizatiti kuwawezesha wakulima kunufaika kupitia kilimo cha kisasa kwa kutumia nyenzo za kisasa na matumizi ya mbegu bora. Tutahakikisha nyenzo hizi zinapatikana kwa wakulima wote na kwa bei nafuu."

Mwaka 2020, Osman alizindua Kampuni ya Grosso Foods B.V. pamoja na shughuli zingine, kampuni hiyo ilijikita katika kuleta mageuzi ya Sekta ya Kilimo Tanzania kupitia njia mbalimbali ikiwamo kuwawezesha wakulima kuongeza mavuno na kupunguza hasara baada ya mavuno na kuboresha upatikanaji wa masoko.

# NMB kuendelea kusaidia ukuaji elimu

**Na Mwandishi Wetu**

MAOFISA wa Benki ya NMB Kanda ya Kaskazini, wamesisitiza dhamira ya benki hiyo kuendelea kusaidia kuweka mazingira rafiki ya kujifunzia shuleni kama sehemu ya kuunga mkono juhudi za kitaifa za elimu bora.

Wakizungumza kwenye kongamano la elimu mjini Tanga wiki iliyopita, viongozi hao waliahidi kuwa NMB itaendelea kushirikiana na mamlaka za mkoa na taifa kuhakikisha viwango vya elimu nchini vinaimarika zaidi.

Meneja Mauzo wa NMB Kanda ya Kaskazini, Innocent Mwanga, alisema katika mahojiano wakati wa kongamano la wadau wa elimu wa Mkoa wa Tanga kuwa kusaidia elimu ni wajibu wa benki hiyo kwa sababu sekta hiyo ni muhimili na nyeti katika maendeleo ya taifa.

"Elimu bora ni suala la msingi katika kujenga jamii na nguvu kazi iliyopevuka kwa ajili ya maendeleo ya sekta mbalimbali za uchumi wa taifa. Ni kwa sababu hiyo Benki ya NMB ilikubali kufadhili kongamano hili ili tuwe sehemu ya juhudi za kusaidia kuboresha viwango vya elimu katika mkoa huu," alisema Mwanga.

Kongamano hilo liliandaliwa na kundi la WhatsApp la Sauti ya Tanga, kwa ajili ya kuchambua changamoto za elimu zinazokabili mkoa huo na kuangalia jinsi ya kuongeza ufaulu wa wanafunzi wa Tanga katika mitihani ya kitaifa.

Naye Meneja wa NMB tawi la Madaraka la jijini Tanga, Elizabeth Chawinga, alisema benki hiyo itaendelea kudhamini kongamano hilo litakalofanyika kila mwaka kama ishara na mfano wa kuendelea kusaidia maendeleo ya sekta ya elimu nchini.

Kwa mujibu wa Mwanga, ushiriki wa NMB katika maendeleo ya elimu umejikita zaidi katika uwekezaji wa kujenga na kuboresha miundombinu hasa kupitia ujenzi wa madarasa na michango ya samani mbalimbali.

Pia, benki hiyo huwafadhili wanafunzi wa shule za sekondari na kutoa suluhisho la bima za elimu kwa ajili ya kulipa ada pale inapotokea walezi kufariki au kupata ulemavu wa kudumu.

Kufadhili elimu ni sehemu muhimu ya shughuli za uwajibikaji wa NMB kwa jamii (CSR) na kila mwaka hutenga asilimia moja ya faida yake baada ya kodi kwa ajili ya uwekezaji huo.

Wakati wa uzinduzi wa Asasi ya NMB Foundation na Programme ya Scholarship na Mentorship ya Nuru Yangu mwezi Septemba mwaka jana, benki hiyo ilisema hutumia zaidi ya Sh. bilioni moja kila mwaka kufadhili masuala ya elimu.

Katika kipindi cha miaka 10 iliyopita uwekezaji mkubwa uliofanyika kwenye elimu ulinufaisha takriban shule 1,400 kote Tanzania kupitia vitu mbalimbali yakiwamo madawati 83,000 na kompyuta 1,200.

"Lengo letu kwa ujumla na nguzo ya msingi katika kuwekeza kwenye elimu ni kuwasaidia watoto wetu kutimiza ndoto zao kwa kuwatengenezea mazingira mazuri ya kujifunzia na kukua kitaaluma," NMB itabainisha kwenye ripoti ya uendeshaji wake ya mwaka 2020.

Akifungua kongamano hilo, Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Adam Malima, aliipongeza benki hiyo kwa kujitolea kwa dhati kusaidia maendeleo ya elimu na kuwataka wadau wengine kuiga mfano wake.

Alisema elimu ni msingi wa maendeleo ya elimu siyo ufaulu tu ila viwango vya ufaulu huo na ubora wa elimu inayotolewa.

Mawazo yake yalisisitizwa na Mwenyekiti wa SAUTI, Mwantumu Mahiza, aliyesema wazo la kuandaa kongamano hilo lilichagizwa zaidi na kutaka kusaidia kuboresha elimu mkoani Tanga.


Ukurasa 12

Zanzibar inavyotoka kiuchumi kupitia uvuvi bahari kuu, mwani, gesi na petroli


Ukurasa 13

**Wananchi kushuhudia shule za ghorofa mijini na vijijini**


Ukurasa 14

**Ali Karume: Tujizatiti kuyatimiza malengo ya Mapinduzi Zanzibar**

siasa

JUMATANO JANUARI 12, 2022

HABARI BORA NA KAMILIFU

Nipashe

MIAKA 58 YA MAPINDUZI ZANZIBAR

# KMKM sasa mwekezaji namba moja bahari kuu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MIAKA 58 ya Mapinduzi ya Zanzibar yaliyotekelezwa Januari 12, 1964 ili kuwakomboa wananchi kutoka ukoloni wa Kisultani, hayatawasahau waasisi wa mapinduzi hayo, akiwamo Rais wa Kwanza wa Zanzibar, Abeid Amani Karume.

Kila mwaka maadhimisho ya mapinduzi hayo yanapofanyika kunakuwa na kauli mbiu na mwaka huu ni uchumi wa buluu kwa maendeleo endelevu na katika kutekeleza kauli mbiu hiyo Kikosi cha Kuzuia Magendo Zanzibar (KMKM) kimezindua uvuvi wa bahari kuu baada ya kununua meli kubwa ya uvuvi au 'trawler.'

Safari ya Kikosi cha KMKM imeanzia mbali na kwamba mara baada ya Mapinduzi mwaka 1964 jukumu la kwanza lililofanywa na chama cha Afroshiraz lilikuwa kuimarisha ulinzi wa bahari kuu kwa sababu Zanzibar ni kisiwa na imezungukwa na bahari, hivyo iliweka mkazo mkubwa kwenye ulinzi wa bahari.

Wakati huo mwaka 1964 KMKM ilikuwa imeunganishwa na kikosi cha idara ya usalama kutokana na umuhimu wa kulinda nchi dhidi ya magendo ya aina mbalimbali kwa wakati huo.

Kwa kikosi hicho haikuwa ni safari rahisi kwa sababu, kilianzishwa kikiwa duni kimafunzo, kiteknolojia na zana za kufanyia kazi lakini baada ya Mapinduzi mwaka 1966, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilikitazama upya kikosi hicho kikaitwa kikosi cha wanamaji na kupatiwa zana za kisasa na kujengewa uwezo kitaaluma.

Mwaka 1973 chini ya uongozi wa Rais wa Pili wa Zanzibar, Aboud Jumbe ndipo alikitangaza kikosi hicho rasmi kuwa ni cha kuzuia magendo badala ya kikosi cha wanamaji wenye dhamana ya kuilinda nchi kiusalama na kupinga magendo ambayo yalikuwa yakidhoofisha uchumi wa Zanzibar.



Mkurugenzi wa Uchumi wa Buluu Hamad Bakari (kulia) akimweleza Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais Dk. Khalid Salum (kushoto) taarifa za jodari mwenye kilo 90 anayeuzwa Sh 990,000, alipozindua uvuvi wa bahari kuu kwenye kikosi cha KMKM. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

**UVUVI BAHARI KUU.**

Baada ya miaka 58 ya kazi KMKM mwaka huu inazindua mradi wa uvuvi wa bahari kuu ,kama sehemu ya maadhimisho ya miaka 58 ya Mapinduzi, kwenye makao makuu ya kikosi hicho Kibweni.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Shughuli za Baraza la Wawakilishi Dk. Khalid Salum Mohammed anapozindua chombo hicho, anasema uchumi wa bluu utainua maisha ya wananchi na uchumi wa taifa kwa sababu Zanzibar ina bahari na endapo samaki watavuliwa kwa wingi na kwa usahihi uchumi utaimarika.

Mohammed anasema Rais Hussein Ali Mwinyi anasisitiza kutumia rasilimali zilizopo kwa maendeleo ya Zanzibar, mali asili ya bahari ni kubwa na ya kutosha na bado haijatumiwa kikamilifu, ndiyo maana amekuja na dhana ya uchumi wa buluu na lazima kumuunga mkono.

Anaongeza kuwa katika uchumi wa buluu kuna bahari, wapo samaki na kilimo kama mwani hivyo samaki wanapovuliwa kwa weledi kutaongeza kipato baada ya kutumia na kusafirisha nje.

Mohammed , anasema baharini kuna rasilimali mafuta na gesi ambayo inachangia ukuaji wa uchumi, kuna usafiri na usafirishaji ambapo sekta hiyo ikitumiwa kikamilifu ina mchango mkubwa katika pato la taifa, ukuaji uchumi na ustawi wa jamii ya Wazanzibari.

"Baharini kuna madini mbalimbali, tunaweza kulima pia, wapo majongoo, samaki aina mbalimbali , tunaweza kufuga kaa yote haya yatawapatia wananchi kipato na fursa za kujikimu kiuchumi,"anasema Waziri Mohammed.

Anasema Rais Mwinyi amekuja na maono makubwa zaidi ya kuvitumia visiwa vidogo vilivyopo Zanzibar kwa ajili ya manufaa ya wananchi na ndiyo maana serikali imekodisha visiwa hivyo kwa ajili ya uwekezaji katika sekta ya utalii.

Anaongeza kuwa katika kuwekeza kwenye visiwa hivyo kikosi cha KMKM kina nafasi kubwa kuhakikisha usalama na kukabiliana na majanga endapo ajali zitatokea akiitaja kazi ya pili kuwa uokozi na kimepatiwa mafunzo ya uokozi na serikali inawategemea katika suala hilo.

"Sisi tumezungukwa na bahari ni visiwa na watu wetu wanafanya shughuli za kiuchumi baharini lakini vilevile usafiri wetu ni majini kwa hivyo mmejipanga zaidi katika suala la uokozi ambayo ni kazi yenu hongereni sana kwa mnavyoifanya,"anasifu Waziri.

Anawakumbusha kuhusu uwekezaji na kwamba ni jukumu la tatu akisema ina faida kubwa ikiwamo kikosi kujimudu kiuchumi na kuwa na fedha za kujiendesha na kuchangia ukuaji wa maendeleo ya taifa na hasa kwenye uvuvi wa bahari kuu.

Katibu Mkuu Tawala za Mikoa na Vikosi Maalumu, Mahfoudh Haji, anasema KMKM kupitia sheria namba moja ya mwaka 2003 ina dhima kubwa ya usimamizi wa ulinzi wa hifadhi ya mipaka ya bahari, ulinzi wa rasilimali na mazingira ya bahari, udhibiti wa uhalifu wa makosa ya baharini, magendo na uokozi wa wahanga wa majanga baharini.

INAENDELEA UK.12

**MIAKA 58 YA MAPINDUZI ZANZIBAR**

# Zanzibar inavyotoka kiuchumi kupitia uvuvi bahari kuu, mwani, gesi na petroli

Na Christina Mwakangale

ZANZIBAR inapotimiza miaka 58 ya Mapinduzi ya Januari 12, 1964, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ), ina matarajio makubwa ya kuinua maisha ya wananchi kupitia uchumi wa buluu, ambao ni uwekezaji baharini ukiwamo uvuvi wa kisasa kwenye bahari kuu.

Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi, Zanzibar, Abdallah Hussein Kombo, anasema pamoja na uvuvi wa samaki watakaouzwa kwenye soko la kitaifa na kimataifa mkakati mwingine ni kulifanya zao la mwani kuwa la kibiashara kwa tija na ulinzi wa mazingira dhidi ya mabadiliko ya tabianchi.

Kombo anayasema hayo akizungumza na Nipashe kwenye mahojiano maalumu kuhusu masuala mbalimbali, yakiwamo mafanikio kiuchumi na changamoto ndani ya miaka 58 ya Mapinduzi, akizungumzia zaidi uwekezaji kwenye bahari kuu. Anaanza kueleza dhana ya uchumi wa buluu, akisema ni masuala ya kiuchumi yanayohusiana na bahari na fukwe zake, eneo la bahari kuu kwenye maji ya kina kirefu, kina kifupi na cha wastani. Kwa ujumla ni fursa mbalimbali za kiuchumi zinazotokana na bahari lakini yote hayo hufanyika kwa kuhusisha ulinzi wa mazingira baharini kwa manufaa ya kizazi cha sasa na kijacho.



Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi, Zanzibar, Abdallah Hussein Kombo akizungumza kwenye moja ya mikutano iliyomkutanisha na wadau wa mazao ya baharini **PICHA: CHRISTINA MWAKANGALE**

**SWALI: Kilimo cha mwani ni shughuli za kiuchumi zinazofanyika baharini, kuna mipango yoyote ya kuwa na kiwanda cha kusindika badala ya kuuza mwani ghafi?**

**JIBU:** Ndiyo, kuna mpango wa kujenga kiwanda hicho kisiwani Pemba, kitakachosimamiwa na Wizara ya Biashara na Viwanda ili kuchochea uzalishaji zaidi wa mwani. Kiwanda cha kusindika mwani ni miongoni mwa mikakati ya wizara ili kuwawezesha wakulima kuongeza kipato cha mauzo ya mwani.

Kitakapokamilika kinatarajiwa kuchakata tani 20,000 kwa mwaka na kwa sasa uzalishaji wa mwani ni tani 8,500 kwa mwaka. Hivyo ni wazi kwamba ujenzi wake utaongeza ajira, kipato cha mtu mmoja mmoja na cha taifa. Zao la mwani pia ni njia muhimu ya kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

> Kiwanda cha kusindika mwani ni miongoni mwa mikakati ya wizara ili kuwawezesha wakulima kuongeza kipato cha mauzo ya mwani.

**SWALI: Unazungumziaje uwekezaji katika uvuvi wa meli kubwa 'fishing trawler' ili kufanikisha uvuvi wa bahari kuu na hatimaye kuinua uchumi wa buluu?**

**JIBU:** Uwekezaji wa uvuvi wa bahari kuu unahitajika. Uvuvi wa aina ya trowler upo katika maji ya bahari ya Tanzania kwa kipindi kirefu, unafanywa na meli za kigeni ambazo zimepata leseni ya kuvua katika bahari kuu ya Tanzania.

Uvuvi huu unaratibiwa na Mamlaka ya Uvuvi wa Bahari Kuu Tanzania (DSFA), hata hivyo wawekezaji zaidi wanahitajika katika uvuvi wa bahari kuu, ili kuifanya Zanzibar kuwa na viwanda vingi vya kuchakata mazao ya samaki. Uvuvi huu, una tija kama kuongeza ajira, kipato kwa wananchi wanaofanya kazi katika kampuni za uvuvi, pamoja na minyororo yake ya thamani. Pia uvuvi huu huongeza pato la taifa kwa kuuza samaki na mazao mengine kwenye soko la kitaifa na kimataifa pamoja.

**SWALI: Uchumi wa buluu unategemea ulinzi na usalama wa mazingira ya bahari, changamoto ya kulinda mazingira ya bahari ikoje katika kipindi hiki ambacho SMZ imeelekeza nguvu kwenye kuvuna mazao ya baharini?**

**JIBU:** Ili uchumi wa buluu ufanikiwe, ni lazima kuwe na udhibiti sahihi wa rasilimali za bahari na fukwe. Hii ni pamoja na uhifadhi wa mazingira yote ya bahari. Ikumbukwe uharibifu wa mazingira ya bahari, unatokana na njia mbili kuu nazo ni mosi, ule unaosababishwa na matumizi mabaya ya rasilimali za bahari, ikiwa ni pamoja na uharibifu wa miundombinu yake kama vile ukataji wa mikoko, kuharibu matumbawe, kuchimba mchanga wa pwani na uvuvi haramu.

Mikakati kwenye uvuvi inawalenga wavuvi wadogo wadogo kupatiwa elimu na zana za uvuvi, ikiwamo boti ili waweze kuvua katika maji makubwa na kuyaacha maeneo tengefu kuwa mazalio ya samaki. Wavuvi, watapatiwa zana sahihi za uvuvi ambazo zitawawezesha kuvua kwa njia salama na kuacha uvuvi haramu. Elimu ya uhifadhi wa mazingira inaendelea kutolewa kwa wakazi wa maeneo ya karibu na fukwe.

Njia nyingine inayochangia uharibifu wa mazingira baharini ni mabadiliko ya tabianchi na kukabiliana na uharibifu huo ni kushirikiana na jumuiya za kikanda na kimataifa katika kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi. Zanzibar kama nchi ya kisiwa, tayari imeanza matayarisho ya namna bora kukabiliana na athari za maabadiliko ya tabianchi.

Miongoni mwa athari za mabadiliko ya tabianchi ni kuongezeka kwa joto na wingi wa maji ya bahari, yaliyosababisha kilimo cha mwani kupungua kutokana na magonjwa yanayoushambulia, Aidha, mazalio ya samaki nayo yameharibika, hivyo kusababisha upungufu wa samaki katika maji madogo. Serikali imewawezesha wakulima wa mwani na wavuvi kwa kuwapatia elimu na boti zinazowapeleka kwenye maji makubwa kufanya kazi zao.

**SWALI: Ni shughuli gani zimefanyika kupitia uwekezaji wa uchumi wa buluu kwenye tasnia za gesi na mafuta? Je, kuna matarajio gani siku za usoni?**

**JIBU:** Kwanza kwenye mafuta na gesi wizara imesimamia matayarisho ya kazi za kuchukua taarifa za mafuta na gesi asilia kwa njia ya mitetemo ya kina ikifahamika kitaalamu kama '3D seismic Survey' kwa lengo la kupata taarifa za kijiolojia na kijiofizikia katika eneo la kitalu cha Pemba - Zanzibar PSA baina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Kampuni ya Maendeleo ya Utafutaji na Uchimbaji wa Mafuta na Gesi Asilia (ZPDC) na Kampuni ya RAKGas Zanzibar Limited.

Kufanya matayarisho ya kupata vitalu vipya kwa ajili ya kutoa leseni kwa maeneo mapya ya uwekezaji, kuiwezesha wizara kukamilisha kuandaa mpango wa uwezeshaji wa wadau wa sekta ya uvuvi wenye thamani ya Shilingi bilioni 169.

Aidha, awamu ya kwanza ya utekelezaji wa mpango, tayari umepatiwa jumla ya Shilingi bilioni 36.5 kutoka IMF, fedha za kuleta ahueni ya janga la COVID 19. Katika mpango huo taratibu za manunuzi na kutoa mafunzo zimekamilika na kinachofuata ni kununua boti za uvuvi 577 zenye mita saba na nane. Aidha, kununua boti 500 za wakulima wa mwani zenye mita tano. Kwa upande wa wafugaji wa majongoo vikundi 100 vitapewa mafunzo kadhalika vikundi 60 vya wafugaji wa kaa navyo vitapata mafunzo na vikundi 40 vya wafuga samaki pamoja na wachakata dagaa kupitia Kampuni ya Uvuvi Zanzibar (ZAFICO) nao watanufaika pia.

Katika mpango huo kuna ujenzi wa soko la kisasa Malindi, kumalizia soko la Tumbe lililoko Pemba na kujenga miundombinu ya uvuvi Unguja na Pemba, kadhalika kuendeleza kituo cha kutotolea vifaranga vya samaki cha Bei-el-Ras na kutayarisha sera mpya ya uchumi wa buluu pamoja na mpango mkakati wake na mpango maalumu wa kuwasaidia wavuvi na wakulima wa mazao ya bahari.

## KMKM sasa mwekezaji namba moja bahari kuu

INATOKA UK.11

Anazungumzia kikosi hicho kuingia katika uvuvi wa bahari kuu akisema siyo tu sehemu ya uzalishaji na kukifanya kujitegemea na kupunguza utegemezi kwa serikali, lakini pia ni sehemu ya kurahisisha utekelezaji wa majukumu ya yake yaliyoainishwa kisheria.

Agosti mwaka jana kikosi hicho kiliingia mkataba na kampuni ya Tijara Marine Service kuvua katika bahari kuu na makubaliano hayo yameiwezesha KMKM kuwa na meli moja kubwa ya uvuvi wa bahari kuu ambayo inaweza kuchukua tani tisa za samaki kwa wakati mmoja.

"Katika kufanikisha kivitendo sera za uchumi wa buluu kikosi, kimelipa zaidi ya Shilingi milioni 122, yakiwa ni malipo mbalimbali ya viza ya wataalamu kutoka Srilanka na leseni ya uvuvi wa bahari kuu na kipo tayari kuanza uvuvi wa bahari kuu kwa sababu wameshapatiwa mafunzo ya vitendo na nadharia kuhusu uvuvi wa bahari kuu." Anasema Haji.

Mkuu wa KMKM, Komodoo Azan Msingiri, anasema uvuvi haramu unarudisha nyuma dhana ya uchumi wa buluu kwa sababu uvuvi huo unaua mazalio ya samaki na samaki wenyewe.

Anaongeza kuwa bila ya kudhibiti uvuvi haramu uchumi wa buluu utakwama kwa sababu ili uwe endelevu lazima mazalio ya samaki yalindwe, yahifadhiwe na kutunzwa wakati wote.

Anaitaja dhamira ya kikosi hicho kuwa ni kumiliki meli nne za uvuvi wa bahari kuu na kushiriki kikamilifu katika uvuvi wabahari kuu na ulinzi katika eneo hilo kwa kushirikiana na mamlaka ya uvuvi wa bahari kuu na kuimarisha mifumo ya uvuvi wa kisasa na kufuatilia mienendo ya vyombo baharini ili kusaidia ulinzi na uokozi baharini.

Msingiri, anasema kikosi hicho tangu kupata meli kubwa ya uvuvi wa bahari kuu kimeshavua zaidi ya tani 10 za samaki wakiwamo jodari ambao wana soko kubwa kitaifa na kimataifa na samaki mwenye kilo 90 ambao huuzwa kwa takribani Shilingi 1,000,000/=.

MAPINDUZI & ELIMU

# Wananchi kushuhudia shule za ghorofa mijini na vijijini

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

ZANZIBAR ikiwa inaadhimisha miaka 58 ya Mapinduzi, inatazama nyuma kuangalia ilikotoka, ilipossimama na inapoelekea baada ya miongo takribani sita ya mapinduzi yaliyomwondoa Sultani Jamshid bin Abdullah na vibaraka wake.

Moja ya malengo ya Mapinduzi ya Zanzibar ni kuwapatia elimu bora watoto wote wa Wazanzibari na hilo jukumu serikali inalibeba ili kulifikia, wananchi wakikumbushwa kuwa kabla ya Mapinduzi ya Januari 12, 1964 zilikuwapo shule 69.

Kati ya hizo mbili zilikuwa za maandalizi wakati 62 ni za msingi na tano za sekondari, lakini kufikia Desemba mwaka jana zimefikia 1,621.

Kufikia Desemba mwaka 2021 Zanzibar ina shule 1, 621, za maandalizi ni 774, wakati za msingi ni 545 na sekondari 302, anasema Rais Hussein Ali Mwinyi, wakati akizindua madarasa ya Shule ya Msingi Sebuleni hivi karibuni.

Anaongeza kuwa idadi hiyo ya shule zilizopo zina wanafunzi 552,328 ikilinganishwa na kabla ya Mapinduzi , shule 62 zilikuwa na wanafunzi 25,432 lakini pia elimu ilikuwa ikitolewa kwa ubaguzi, Waafrika wakiwekwa kando. Ndiyo maana Mapinduzi yanalenga kuwapa elimu bora bila ubaguzi.

Mwaka 1964 Rais wa Kwanza wa Zanzibar, Abeid Amani Karume anatangaza mpango wa elimu bure kwa wote bila ya ubaguzi wa rangi, dini au kabila.

Licha ya ongezeko la shule za serikali zilizopo Zanzibar baada ya Mapinduzi , kumekuwa na msongamano mkubwa wa wanafunzi madarasani hali inayochangia kushusha ufaulu wa wanafunzi katika mitihani ya taifa, anasema.

Katika kutatua changamoto hizo na nyingine za sekta ya elimu Serikali ya Zanzibar, inatarajia kujenga shule za ghorofa na za kisasa, anasema Rais Mwinyi, akieleza kuwa idadi kubwa inatokana na kuongezeka kwa idadi ya watu nchini na kukua kwa maeneo ya makazi.

Hali hiyo kwa mujibu wa Rais, inasababisha kuongezeka kwa mahitaji ya majengo ya shule na madarasa na idadi ya wanafunzi kila mwaka.

Anasema ujenzi wa shule hizo utapunguza msongamano wa wanafunzi madarasani ili kila mmoja apate haki ya elimu katika mazingira bora bila kujali anaishi mjini au kijijini.

Aidha, anasema serikali itazifanyia ukarabati shule za msingi na sekondari pamoja na ujenzi wa vyoo 1,963 kwenye shule za Unguja na Pemba na ujenzi wa nyumba 10 za walimu na kununua madawati 8,000 kwa ajili ya wanafunzi 24,000 wa shule za msingi ambao baadhi yao wanakaa sakafuni.



Rais wa Zanzibar, Hussein Ali Mwinyi, ameahidi kujenga shule za ghorofa vijijini na mijini. **PICHA ZOTE: MTANDAO**



Shule ya Sekondari ya JKU moja ya shule za ghorofa visiwani Zanzibar.

**MAFANIKIO YAKUJIVUNIA**

Akizungumzia baadhi ya maendeleo ya elimu kwa miaka 58 ya Mapinduzi, Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Simai Muhammed Said, anasema ni kuimarika kwa fursa za sekta hiyo.

> Kuanzia mwaka 2017 michango ya wazazi iliondolewa pia katika ngazi ya sekondari kwa shule zote za serikali.

Serikali inaimarisha taasisi ya sayansi na teknolojia ya Karume ili ichangie kutoa wahandisi wa kuhudumia ndege na marubani kwa ajili ya kurusha ndege na kuinua sekta ya usafiri na usafirishaji wa anga, anasema Waziri Said.

Anasema wizara inaendelea kuwarejesha watoto wote waliotoroka shule na kwamba wanafunzi 2,609 wakiwamo wanawake 631 na wanaume 1,973 wamerejeshwa shuleni kati ya watoto 35,732 walio nje ya shule kwa sababu za kutopelekwa shule au kutoroka kutokana na sababu mbalimbali.

Waziri Said anaeleza kuwa katika kuhakikisha elimu inapatikana kwa watoto wote wa Zanzibar, mwaka 2015 serikali ilifanya maamuzi ya kuondoa michango ya wazazi katika elimu ya maandalizi na msingi kwa shule zote za serikali.

"Kuanzia mwaka 2017 michango ya wazazi iliondolewa pia katika ngazi ya sekondari kwa shule zote za serikali,"anakumbusha

Simai na kusema kuwa sambamba na hatua hizo serikali imezipatia shule vifaa vya kujifunzia kama vitabu , vifaa vya maabara za sayansi na maktaba pamoja na vitabu.

Anaeleza kwamba katika kuimarisha mazingira bora ya elimu serikali imenunua viti na meza 35,610 kwa ajili ya sekondari na madawati 42,620 kwa shule za msingi.

**CHANGAMOTO**

Waziri Said anasema miongoni mwa changamoto zinazoikabili sekta ya elimu Zanzibar ni ufaulu mdogo wa wanafunzi katika masomo ya sayansi na hisabati.

Anasema hali hiyo inatishia na imechangiwa na uhaba wa walimu wa masomo hayo, uhaba wa maabara katika shule za sekondari na vifaa vya kujifunza kwa vitendo (practical).

"Katika kutatua changamoto hii serikali imeweka moja ya vipaumbele vyake ni kuimarisha ufundishaji wa masomo ya sayansi na hisabati kama fizikia, kemia na baiolojia na kuongeza upatikanaji wa elimu wa kufundisha masomo hayo," anasema.

Anaeleza kuwa imani yake baada ya serikali kutekeleza jukumu hilo wanafunzi watafanya vizuri katika masomo yao hasa ya sayansi na ufaulu wao kuongezeka.

"Uhaba wa miundombinu ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) ni changamoto nyingine hali inayopelekea matumizi madogo ya teknolojia hiyo katika elimu na uhaba wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia vya wanafunzi wenye mahitaji maalumu."

Anaahidi kuwa serikali itaendelea kuzitafutia ufumbuzi changamoto zote katika sekta ya elimu na kuhakikisha malengo ya Mapinduzi ya kupata elimu bora kwa watoto wote wa Wazanzibari yanafikiwa.

## MIAKA 58 YA MAPINDUZI ZANZIBAR

JUKWAA LA VIONGOZI

# Ali Karume: Tujizatiti kuyatimiza malengo ya Mapinduzi Zanzibar



Balozi Ali Karume. **PICHA: MTANDAO**

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAKATI Zanzibar inaadhimisha miaka 58 ya Mapinduzi yaliyoasisiwa na Rais wa kwanza Abeid Amani Karume, mtoto wake Balozi Ali Karume, anakumbusha suala la ardhi na makazi bora kwa Wazanzibari kuwa ndilo hasa lilikuwa lengo la mapinduzi hayo.

Ali mtoto wa pili kuzaliwa katika familia ya Mzee Karume, anazungumza na Nipashe katika mahojiano huko nyumbani kwake Maisara mjini Zanzibar, anakumbusha kuwa miaka 58 ya Mapinduzi, yaliyofanyika mwaka 1964 yatakuwa endelevu iwapo yanabakia kuwapatia wananchi makazi bora pamoja na ardhi kwa ajili ya kilimo, uwekezaji na kuinua maisha yao.

Balozi Ali aliyezaliwa mwaka 1950, wakati wa Mapinduzi alikuwa na miaka 14 na anakumbuka namna ambavyo baba yao alitamani maisha bora kwa kila Mzanzibari akieleza kusikitishwa kwake kwa sababu malengo hayo yameanza kupotea kwa sababu ardhi imekuwa ikimilikishwa kwa raia wa kigeni tena kinyume na sheria.

"Mfano sheria ya Tanzania

> "Malengo muhimu ya Mapinduzi ya Zanzibar yaliyowasukuma waasisi kuung'oa utawala wa kisultani ni umiliki wa ardhi kwa maendeleo ya kilimo na makazi bora kwa wananchi wazalendo.

Bara ipo vizuri na hairuhusu raia wa kigeni kumiliki ardhi kwa sababu ardhi ndiyo uti wa mgongo wa uchumi wa nchi na ni mali ya serikali, "anakumbusha.

Aidha, anasema malengo muhimu ya Mapinduzi ya Zanzibar yaliyowasukuma waasisi kuung'oa utawala wa kisultani ni umiliki wa ardhi kwa maendeleo ya kilimo na makazi bora kwa wananchi wazalendo.

Anasema suala la ardhi lilikuwa moja ya vipaumbele vya msingi vya kwanza kwa sababu kabla ya mapinduzi ardhi ilikuwa ipo katika mikono ya familia na ukoo wa Sultani ikiwamo ile yenye rutuba kwa shughuli za kilimo.

Anaongeza kuwa Baba yake au Mzee Karume aliwatangazia Wazanzibari katika mkutano wa kwanza wa hadhara baada ya mapinduzi kwamba ardhi yote iliyokuwa ikimilikiwa na watawala wa Kisultani na familia zao na ukoo wao sasa itachukuliwa na kuingia katika mikono ya serikali kwa ajili ya kugawiwa kwa wananchi wote.

Anaeleza kuwa mwaka 1965 zoezi la kugawa ardhi ya ekari tatu lilianza kwa shamba ambalo lilikuwa likimilikiwa na familia ya Kisultani huko Dole na wananchi kumilikishwa kama serikali ilivyowaahidi.

Anawataka wananchi kuacha kuuza maeneo au ardhi yao kwa wageni kwa sababu ardhi ndiyo utajiri na ikiwezekana kuingia ubia na wageni hao, lakini si kuwapa haki miliki.

Balozi Karume anasema mapinduzi ya Januari 12 ndiyo yaliyowakomboa wananchi wa Unguja na Pemba kuwa huru katika nchi yao na kusema uhuru wa Desemba10 mwaka 1963 ulikuwa bandia na haukuwa na maslahi kwa wananchi wala taifa hilo.

Anasema uhuru bandia kwa kiasi kikubwa uliongeza ari kwa chama cha ASP kufanya kila mbinu kuona wananchi wazalendo wanakuwa huru katika nchi yao na ndiyo sababu ya kufanyika kwa mapinduzi ya Januari 12 mwaka 1964.

Aidha Karume, anaeleza kufurahishwa na uamuzi uliochukuliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya kuwatambua kwa mujibu wa sheria viongozi waasisi wa mapinduzi ya Zanzibar ambao walifanya kazi kubwa katika kuleta ukombozi wa Zanzibar.

Anasema ni uamuzi sahihi ambao unastahili kupongezwa na kuungwa mkono na nguvu zote ambao tafsiri yake nyepesi ni kutambua mchango wa viongozi katika ukombozi wa Zanzibar.

"Ujumbe wangu tuyaenzi mapinduzi ndiyo yaliyoleta Uhuru wa Zanzibar lakini Muungano ndiyo uliotuunganisha sote na kuwa taifa moja chini ya mwamvuli wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,"anasema.

Balozi Karume ambaye baba yake aliuwawa April 1972, anasema malengo makubwa ya mapinduzi ni kuweka hali za wananchi sawa na kuishi katika nchi yao na kupata fursa zote wanazostahiki.

Anasema ndiyo maana baada ya Mapinduzi ya Zanzibar Sheikh Karume alitangaza kupiga marufuku shule zote zilizokuwa zikitoa elimu kwa misingi ya ubaguzi na baadaye kutangaza elimu bure kwa wananchi wote Septemba 23 mwaka 1964.

Balozi Karume anaeleza kufurahishwa na awamu zote zilizopata kushika nafasi ya kuongoza Zanzibar kuendelea kutekeleza sera ya elimu bure huku elimu ya maandalizi ikitangazwa kuwa ya lazima kwa mujibu wa sera ya elimu ya Zanzibar.

"Elimu ndiyo msingi muhimu wa maendeleo kwa taifa lolote ambapo hayo mataifa yaliyopiga hatua kubwa katika sayansi na teknolojia msingi wake ni elimu." anasema.

**KUHUSU SIASA**

Balozi Ali Karume hata sasa ni mwanasiasa na mwaka 2015 alionyesha nia ya kugombea urais wa Tanzania wakati 2010 alitupa karata akitaka kugombea urais wa Zanzibar na katika CCM ni mjumbe wa Halmashauri Kuu ya Chama Mkoa wa Kusini Magharibi.

Akiwa mwanadiplomasia ameiwakilisha Tanzania katika nchi mbalimbali za Ulaya, Marekani,Ubelgiji, Italia na Ujerumani, anazungumzia masuala ya siasa kwamba kwa miaka 58, demokrasia Tanzania imekuwa kwa kasi kubwa.

Anaongeza kuwa amekuwa balozi wa nchi mbalimbali duniani lakini kwa Tanzania kuna demokrasia bora akilinganisha na mataifa mengine ambayo amefanyia kazi.

Anakumbusha kuwa tangu mwaka 1992 ulipoanzishwa mfumo wa vyama vingi Tanzania, demokrasia imeimarika kwa sababu kila baada ya miaka mitano imekuwa ikifanya uchaguzi mkuu ambao unashirikisha vyama tofauti vya siasa na wapiga kura huchagua viongozi wanaowataka lakini nchi nyingine mfano Afrika Kusini, rais anachaguliwa na bunge.

Anaeleza kuwa tangu kuanza mfumo wa vyama vingi inasikitisha baadhi ya viongozi kuzembea katika masuala nchi inavyoendeshwa kwa kulegeza maadili ya mapinduzi ikiwamo suala la kuwapatia raia ardhi.



# DC awataka wananchi kuweka akiba chakula

**Na Ibrahim Joseph,** KONGWA

MKUU wa Wilaya ya Kongwa, Remidius Emmanuel, amewataka wananchi kutunza chakula kutokana na hali ya ukame iliyojitokeza msimu huu wa kilimo.

Emmanuel alitoa agizo hilo jana alipozungumza na Nipashe kuhusu hali ya chakula kwenye wilaya hiyo kutokana na kuchelewa kunyesha kwa mvua katika msimu huu wa kilimo.

Kutokana na kuwapo kwa tishio la ukame, mkuu huyo wa wilaya aliwataka wananchi kutunza chakula.

"Tulizoea tarehe kama hizi wananchi wanakuwa wameshaanza kuvuna baadhi ya mazao waliyolima shambani, lakini kwa sasa hatujui mvua zitaanza kunyesha lini. Hali hii ni hatari tunatakiwa kutunza chakula tulichonacho," alisema.

Alisema, kutokana na hali ya uhaba wa mvua msimu huu wananchi wanatakiwa kuanza kutunza chakula ili kuchukua tahadhari ya kukabiliwa na njaa mwaka huu.

Alibainisha kuwa misimu mingine ya nyuma ya kilimo iliyopita mvua zilikuwa zinaanza kunyesha kuanzia Desemba, lakini kwa msimu huu, mpaka sasa wako wananchi ambao bado hawajapata kabisa au kutifua mashamba yao.

Kadhalika, alizuia matumizi ya mtama na mahindi kutengenezea pombe kwa sababu wanapunguza akiba ya chakula.

Alisema kutokana na hali ya ukame uliopo unatishia hali ya chakula katika eneo hilo kwa sababu haijulikani mvua itanyesha lini.

Pia aliwataka wananchi kulima mazao yanayostahili ukame kwa sababu hata mvua zikinyesha zitakuwa chini ya wastani.

Aliongeza kuwa wilaya hiyo inaendesha kampeni ya kuwataka wananchi kulima alizeti, mtama, uwele na mazao yanayohitaji mvua chache ili kuepuka kuingia kwenye njaa mwaka huu.

Emmanuel aliwataka wakulima kulima mazao hayo yanatostahimili ukame kabla ya mazao mengine ya biashara kama mahindi ili kuzitumia mvua za msimu huu vizuri.

Hata hivyo aliwataka wakulima kuwatumia maofisa ugani waliopo kwenye maeneo yao ili kuepuka kulima mazao yasiyostahimili hali ya hewa kwenye maeneo hayo.

# Bashungwa aanika kipaumbele TAMISEMI

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Innocent Bashungwa, amesema kipaumbele cha serikali ni kushughulikia changamoto za wananchi kuanzia ngazi ya kijiji.

Akizungumza na menejimenti ya TAMISEMI juzi muda mfupi baada ya kuapishwa katika Ikulu ya Chamwino, Dodoma, Bashungwa alisema wataalamu wanatakiwa kuangalia kero zilizoko kwenye vijiji ili kupata picha halisi ya matatizo yanayowakabili wananchi na kupanga mipango ya kimkakati katika kuzitatua.

"Ninawataka watumishi wa Ofisi ya Rais TAMISEMI, kujikita zaidi kwenye matatizo yanayojitokeza zaidi kwenye vijiji na kuyachukulia kuwa ni changamoto ya nchi nzima, hivyo tunahitajika kuweka mikakati ya kuzitatua na kuwezesha wananchi katika kutoa huduma bora," alisema Bashungwa.

Alibainisha kuwa watumishi wanapaswa kujifunza kwenye ngazi za vijiji ili kero wanazopata wananchi zikiwamo ukosefu wa madarasa, zahanati na mengineyo zitatuliwe haraka iwezekanavyo.

Waziri Bashungwa alisema utatuzi wa kero hizo utasaidia kutoa huduma bora kwa wananchi na kuzingatia hilo wakati wa uandaaji wa bajeti za kila mwaka kwenye wizara husika.

Pia aliwataka wataalamu ngazi ya mamlaka za serikali za mitaa kuhakikisha wanafanya tathmini na ufuatiliaji wa miradi ya maendeleo kwa kuangalia uhalisia wa fedha zilizopelekwa na thamani ya miradi inayotekelezwa hasa katika ngazi za vijiji ili kupata uhalisia wa matumizi ya fedha zinazotolewa na serikali.

Bashungwa alimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kumteua kushika wadhifa huo na kuahidi kuwa atatimiza wajibu wake kwa kushughulikia kero mbalimbali za watumishi na wananchi.

Kadhalika, alisisitiza matumizi ya mifumo kwa watumishi wote wa mamlaka za serikali za mitaa itakayorahisisha ufuatiliaji na utendaji kazi ili kupata taarifa za utekelezaji wa miradi kwa wakati.

Naibu Waziri wa Ofisi ya Rais TAMISEMI, anayeshughulikia Elimu, David Silinde, aliwataka watumishi kuongeza ushirikiano katika utekelezaji wa majukumu yao ili kutatua kero za wananchi na kutoa huduma bora kwa jamii.

Naibu Waziri Ofisi ya Rais-TAMISEMI, anayeshughulikia Afya, Dk. Festo Dugange, alimwahidi Waziri Bashungwa kuwa watampa ushirikiano wa kutosha katika utekelezaji wa majukumu yake.

Naye Katibu Mkuu TAMISEMI, Prof. Riziki Shemdoe, alisema kwa ushirikiano mkubwa wa watumishi kwa sasa umefanyika ujenzi wa madarasa 15,560, vituo vya afya 233 huku miradi mbalimbali ikitekelezwa.



Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye (katikati), akizungumza na menejimenti na watumishi wa wizara hiyo, baada ya kuwasili ofisini kwake, katika Mji wa Serikali Mtumba, jijini Dodoma jana. Kulia ni Naibu Waziri wa Wizara hiyo, Mhandisi Kundo Mathew na Katibu Mkuu wa Wizara, Dk. Jim Yonazi. **PICHA: WIZARA YA HABARI**

# Prof. Mkenda akiri ana mzigo mzito

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WAZIRI wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, amesema wizara aliyopewa ni ngumu kulinganisha na ile ya kilimo ambayo ametoka kuiongoza.

Pamoja na hayo, amewataka watumishi wa wizara kufanya kazi kwa ushirikiano ili kuhakikisha wanainua elimu nchini.

Akizungumza juzi wakati wa mapokezi katika wizara hiyo, Prof. Mkenda alisema Wizara ya Kilimo si ngumu kama ya elimu kwa sababu kilimo kila mtu analima anavyoweza tofauti na elimu. Mkenda alisema kuwa elimu iko kila mahali, hivyo watu wanapaswa kufanya kazi kwa bidii ili kusonga mbele.

"Nawashukuru kwa mapokezi yenu, nimeyafurahia. Sijawahi kukutana nayo katika wizara nilizofanya kazi. Mapokezi haya yakawe chachu ya utendaji kazi," alisema Prof. Mkenda.

Waziri Mkenda alimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan, kuendelea kumwamini kuiongoza wizara hiyo ambayo aliahidi ataisimamia vizuri.

Alisema lengo lake ni kuona elimu inakwenda juu badala ya kushuka chini katika maeneo mbalimbali.

Hata hivyo, aliwataka wafanyakazi wasiogope kutoa uamuzi mgumu pale unapohitajika kufanywa ili kusaidia kuinua juu elimu.

Aliwataka pia wakafanye kazi bora ya elimu kwa sababu wana jukumu kubwa la kufanya ili wasonge mbele katika kuinua elimu.

Naye Katibu wa Wizara hiyo, Prof. Eliaman Sedoyeka, aliwashukuru wafanyakazi wa wizara hiyo kutokana na mapokezi mazuri walioonyesha kwa waziri na wateule wengine.

Alisema kinachotakiwa ni kwenda kufanya kazi kwa bidii ili kuhakikisha elimu inasonga mbele na kwamba kazi ndio msingi bora wa kuendeleza elimu nchini.



# Watatu matatani tuhuma za mauaji ya ndugu yao

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

JESHI la Polisi mkoani Mbeya, linawashikilia watu watatu kwa tuhuma za mauaji ya ndugu yao, Peter Mwakitalima (40), mkazi wa Mitete, Rungwe mkoani Mbeya.

Wanaodaiwa kuhusika na mauaji hayo ambao wanashikiliwa ni Musa Mwakitalima (39) Mkazi wa Kibisi, Ipyana Kakina (36), Hellen Ihojo (34).

Kaimu Kamanda Mkoa wa Mbeya, Christina Musyani, aliwaambia waandishi wa habari kwamba tukio hilo lilitokea Januari 9 majira ya saa 6:00 mchana. Alisema marehemu Mwakitalima aliuawa kwa kukatwa na shoka kichwani akiwa nyumbani kwake.

Musyani alisema kati ya watuhumiwa watatu waliohusika na mauaji hayo, wawili ni ndugu wa marehemu Mwakitalima. Alisema chanzo cha mauaji hayo ni mgogoro wa ardhi kati ya marehemu na wadogo zake baada ya baba yao kufariki dunia na kuwaachia mali ambayo ni nyumba.

"Ndugu hao walipanga njama kumuua ili kumiliki mali hizo ambao Mwakitalima alikuwa anazisimamia. Natoa pole sana kwa familia, naahidi watuhumiwa watashughulikiwa kwa mujibu wa sheria za nchi," alisema Musyani.

Katika hatua nyingine, jeshi hilo kwa kushirikiana na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) Wilaya ya Kyela, linamsaka mtuhumiwa aliyefahamika kwa jina moja la Benny, Mkazi wa Kyela mkoani Mbeya kwa tuhuma za kuingiza nchini bidhaa zilizopigwa marufuku aina ya Ice Dry London Gin maboksi mawili na katoni 30 za sukari.

Bidhaa hizo, alisema Musyani kwamba zilikamatwa Januari 9, mwaka huu, majira ya saa 12:00 jioni katika eneo la Kilambo baada ya Jeshi la Polisi kwa kushirikiana na TRA kupata taarifa za siri juu ya uingizwaji wa bidhaa hizo na kuanza msako ambao ulifanikisha kuzikamata.

Musyani alisema bidhaa hizo zilikutwa zimehifadhiwa katika stoo nyumbani kwa mtuhumiwa ambaye alitoroka baada ya kuwaona askari na maofisa wa TRA na kwamba msako unaendelea kumtafuta.



Mkurugenzi wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI), Kituo cha Uyole, Dk. Tulole Bucheyeki (kulia), akiwaelekeza wakulima wa Wilaya ya Rungwe, namna bora ya matumizi bora ya mbegu katika moja ya shamba la mkulima wilayani humo jana. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

## CCM yapongeza ujenzi madarasa

**Na Grace Mwakalinga,** SONGWE

KAMATI ya Siasa ya Chama Cha Mapinduzi CCM, Wilaya ya Mbozi mkoani Songwe, imewapongeza watumishi wa wilaya hiyo kujitahidi kukamilisha ujenzi wa miradi ikiwamo vyumba vya madarasa.

Katibu Mwenezi wa CCM Wilaya ya Mbozi, Zawadi Shombe, alitoa pongezi hizo jana baada ya ukaguzi wa miradi ulioanza Januari 4, mwaka huu. Kati hiyo ilifanya ziara katika miradi ya ujenzi wa miundombinu ya maji, vyumba vya madarasa na vituo vya afya.

Shombe alisema kamati ya siasa iliridhishwa na kasi ya ujenzi wa miradi hiyo ambayo inasimamiwa na serikali kwa kushirikisha nguvu kazi ya wananchi.

"Miongoni mwa miradi tuliyoitembelea ni pamoja na ujenzi wa Shule ya Sekondari ya Igamba inayojengwa katika kijiji cha Msanyila, shule ambayo inajengwa kwa fedha za ndani kwa zaidi ya Sh. milioni 100," alisema Shombe.

Aidha, Shombe alisisitiza watumishi wa Wilaya ya Mbozi kuzingatia matumizi sahihi ya fedha na kuhakikisha thamani ya fedha inaendana na ujenzi wa miradi iliyotekelezwa.

Katika hatua nyingine, kamati hiyo ilitoa pole kwa familia ya kijana aliyefahamika kwa jina la Ben Mtafya aliyekuwa akikatisha tiketi katika stendi ya Vwawa wilayani Mbozi ambaye alifariki dunia baada ya kujinyonga kwa kutumia mkanda katika msitu wa Jamatini.

Kwa mujibu wa taarifa ya Kamanda wa Polisi Mkoa wa Songwe, Janeth Magomi, chanzo cha kijana huyo kujinyonga hakijafahamika kwa sababu hakuna ujumbe wowote aliouacha na kwamba upelelezi unaendelea kubaini chanzo.

# Tembo wavamia makazi ya watu, wala mazao

**Na Grace Mwakalinga,** MBARALI

MAKUNDI ya tembo kutoka Hifadhi ya Taifa ya Ruaha, yameingia katika makazi ya wananchi katika Kata ya Igava wilayani Mbarali na kuvunja nyumba za watu kisha kula akiba ya chakula.

Kutokana na hali hiyo, wananchi hao wameiomba serikali kusaidia kukabiliana na makundi ya tembo ambao wanavamia makazi na kufanya uharibifu.

Wananchi hao walitoa kilio hicho juzi mbele ya wadau wa uhifadhi wakiwamo Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA), Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori (TAWA) na Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori (TAWIRI) ambao walifika katika kata hiyo kwa lengo la kutoa elimu ili kukabiliana na uvamizi wa tembo hao.

Mmoja wa wananchi hao, Kalaika Karashi, alisema tembo wamekuwa kero kwao kwa kuwa kwa sasa hakuna mazao shambani, hivyo wanaenda kwenye makazi ya watu kisha kuezua nyumba za nyasi na kuvuta vyakula na kuanza kula.

"Kuna uvamizi mkubwa wa tembo hapa. Wanafika hadi kwenye makazi yetu kisha kula vyakula vilivyohifadhiwa ndani. Tunaishi kwa wasiwasi sana, tunaomba mamlaka zinazohusika zinatusaidia kuondoa wanyama hawa," alisema Karashi.

Naye Henry Mkomole alisema sababu kubwa iliyochangia tembo kuvamia makazi ya watu ni upanuzi wa Hifadhi ya Ruaha hali inayosababisha wanyama kuishi karibu na wananchi na kuhatarisha maisha yao.

Alisema tembo ni wanyama wakatili na wanaweza kusababisha madhara kwa binadamu, hivyo alishauri kuandaliwe utaratibu maalum wa namna ya kudhibiti wanyama hao.

Kilio cha wananchi hao kilizifikisha mamlaka zinazohusika na usimamizi wa wanyama na uhifadhi, kufika Kata ya Igava na kuanzisha vikundi vya vijana kwa ajili ya kufukuza tembo sambamba na kuwafundisha wananchi mbinu za kukabiliana na tembo bila kuleta madhara kwa pande zote mbili.

Ofisa Uhusiano wa Hifadhi ya Taifa ya Ruaha, Shariff Yassin, alisema wamewafundisha wananchi mbinu za kukabiliana na tembo hao bila kudhurika.

Aliwaomba wananchi kuzingatia mbinu hizo ili kuepukana na madhara yanayoweza kutokea ikiwamo uharibifu wa mazao na vifo.

Ofisa Mfawidhi kutoka TAWA, Dorine Ulomi, alisema wataendelea kutoa elimu kwa wananchi ili kukabiliana na uvamizi wa tembo katika makazi yao na kuwasisitiza kutoa taarifa pindi wanaoona uharibifu.

Akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Wilaya ya Mbarali, Reuben Mfune, Magdalena Sikwese, aliwasisitiza wananchi kuendelea kuchukua tahadhari ili kukabiliana na tembo hao.

Diwani wa Igava, Nassoro Udesi, aliwasisitiza vijana waliopata mafunzo ya namna kukabiliana na tembo kupitia mbinu mbalimbali kuwasaidia wananchi wengine ili kuwa salama.



## Kasi ya maendeleo yaongeza mahitaji ya sekta ya elimu

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

RAIS mstaafu wa Zanzibar, Dk. Amani Abeid Karume, amesema kasi ya maendeleo imesababisha mahitaji ya elimu kuongezeka na kufanya serikali kuelekeza nguvu zaidi katika sekta ya elimu.

Akizungumza baada ya kufungua madarasa manane ya Shule ya Sekondari Nungwi, Kaskazini Unguja, alisema fani yoyote duniani inahitaji elimu, hivyo kuweka mazingira bora kutasaidia kujenga ushawishi kwa wanafunzi kufuatilia masomo yao.

Karume alisema kwa kutambua umuhimu wa suala hilo, serikali ilitangaza elimu bure baada ya Mapinduzi ya Zanzibar, hivyo dhamira hiyo iendelee kufanya kazi kwa kujenga mazingira bora ya kielimu.

Dk. Karume aliwataka wazazi na walezi kusimamie watoto wao katika kupata elimu ili malengo hayo ya mapinduzi kufanikiwa.

Alisema kabla ya Mapinduzi ya Zanzibar, elimu ilitolewa kwa ubaguzi na ndipo mwasisi wa Mapinduzi, Hayati Abeid Amani Karume, alitangaza elimu bure ili kila mmoja kupata fursa hiyo.

Naye Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Simai Mohammed Said, alisema maendeleo ya elimu yatafikiwa kwa wananchi kuwa tayari katika kushirikiana kati ya wadau na serikali ili kuifanyia kazi dhamira ya mapinduzi.

Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Ali Khamis Juma, alisema ongezeko la idadi ya wanafunzi limesababisha kuimarishwa mazingira ya kujifunza ili kuongeza nguvu katika masomo na kutoa wataalamu.

Alisema ujenzi huo utapunguza msongamano wa wanafunzi madarasani na kuongeza ufaulu wao shuleni hapo.

Ufunguzi huo ni miongoni mwa shamrashamra za miaka 58 ya Mapinduzi ya Zanzibar ambayo kilele chake ni leo.

# Kiwanda chalia gharama malighafi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

KIWANDA cha Nguo Zanzibar kinakabiliwa na kero ya gharama ya ununuzi wa usafirishaji wa makaa ya mawe kwa ajili ya uzalishaji ambayo huagizwa nje ya Zanzibar.

Mwakilishi wa kiwanda hicho, Juma Reli, alisema hayo jana wakati akizungumza katika uzinduzi wa kiwanda hicho, Chumbuni Zanzibar.

Alisema matatizo mengine ni gharama za umeme kwa ajili ya kuendesha kiwanda na bidhaa za viwanda vya ndani kutopata soko.

Reli alisema changamoto hizo zikifanyiwa kazi, zitasaidia kushindana katika mazingira sawa na viwanda vya Tanzania na Afrika Mashariki.

Alisema mradi huo unamilikiwa na familia ya mwekezaji kutoka nchini Kenya na uzalishaji wake ni nguo na umegharimu dola milioni 53 na kinazalisha mita 200,000 za vitambaa vikiwamo vya malighafi ya pamba.

Kwa mujibu wa mwakilishi huyo, bidhaa zinazozalishwa kiwandani hapo ni vitenge, kanga, madera na bidhaa zingine kwa ajili ya mavazi.

Alisema wafanyakazi wa kiwanda hicho wamepata mafunzo na ujuzi wa kutumia mashine za kisasa kutoka kwa wataalamu wa China na wana wataalamu 16 kutoka China.

Pia alisema kiwanda kimeajiri wafanyakazi 321 na kimeongeza fedha za kigeni, pato la taifa na kupunguza uagizaji wa bidhaa kutoka nje ya nchi.

Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharibi, Idrisa Kitwana, alisema kufunguliwa kwa kiwanda hicho ni faraja kubwa katika kuhakikisha wananchi wanapata ajira.

Alisema uwapo wa kiwanda hicho kitazaa ajira zingine ndogo kwa wajasiriamali kwa sababu bidhaa zinazozalishwa watazisambaza sehemu zingine.

Mbunge wa Chumbuni, Ussi Pondeza, alisema kiwanda hicho kiko ndani ya jimbo hilo na alimpongeza mwekezaji kwa sababu vijana wa jimbo hilo wamepata fursa ya ajira kwa asilimia 30.

Naye Mwakilishi wa jimbo hilo, Miraji Kwaza, alisema licha ya asilimia 30 ya ajira pia pato la ukuaji wa uchumi wa nchi litapatikana kutokana na kiwanda hicho.

Naibu Katibu Mkuu wa CCM Zanzibar, Abdallah Mabodi, alimpongeza Rais Samia Suluhu Hassan ambaye alizindua kiwanda hicho kwa utekelezaji wake mzuri wa ilani ya uchaguzi ya chama na kuendelea kukopa fedha kwa maslahi ya taifa ili uchumi wa nchi ukue.

Alisema uzinduzi huo utatoa ajira ambazo zitakuwa miongoni mwa ajira 300,000 alizoziahidi Rais Dk. Hussein Mwinyi wakati wa kampeni zake.

" Mapinduzi ya ukombozi yamekwisha na sasa ni mapinduzi ya kimaendeleo," alisema naibu huyo.

Uzinduzi wa kiwanda hicho ni sehemu ya shamrashara za miaka 58 ya Mapinduzi ya Zanzibar ambazo zinafikia kilele leo.



Mkuu wa Wilaya ya Iringa, Mohamed Moyo (kushoto), akiongoza dua ndogo ya kumwombea aliyekuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Zanzibar anayeshughulikia Muungano na mwanasiasa mkongwe, marehemu Hassan Nassor Moyo, walipotembelea kaburi lake katika Mtaa wa Fuoni, Zanzibar jana, ikiwa ni shamrashamra kuelekea miaka 58 ya Mapinduzi ya Zanzibar. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Hospitali yaandaa kitengo cha matibabu ya wazee

**Na Mwandishi Wetu**

UONGOZI wa Hospitali ya Kivunge iliyoko mkoa wa Kaskazini Unguja, umesema umekusudia kuanzisha kitengo maalumu cha matibabu kwa ajili ya wazee ili kuwapatia huduma bora bila usumbufu.

Akizungumza baada ya Jumuiya ya Wazee Wastaafu (JUYAWAZA) Zanzibar kufika hospitalini hapo, Katibu wa Hospitali hiyo, Fatma Khatib Haji, alisema hatua hiyo ya uazishwaji wa kitengo hicho imekuja baada ya kugundua wazee wengi wanaofika hospitali hiyo wanakabiliwa na maradhi ambayo yanahitaji uangalizi wa hali ya juu pamoja na busara katika kuwatibu.

Alisema hatua hiyo italeta mabadiliko na maendeleo zaidi katika kuimarisha ustawi wa wazee hao ambao wanakabiliwa na magonjwa ya viungo kama miguu, mgongo, macho na shinikizo la damu.

Fatma aliiomba Wizara ya Afya Zanzibar kuongeza nguvu katika mpango huo ili kufanikisha azma ya uongozi katika kuwasaidia wazee, kutoa matibabu bora na yenye uhakika kwa utoaji wa vifaa tiba, dawa na kupewa jengo maalumu kwa ajili ya wazee.

Mwenyekiti wa JUWAZA, Hashim Bakari Kondo, alisema jumuiya imekuwa ikifanyakazi kubwa katika kuwasaidia wazee hasa wale wa majumbani katika kuwatafutia huduma za matibabu.

Alisema licha ya serikali kutoa huduma bora kwa wananchi wake, bado wazee wanakabiliwa na maradhi, hivyo wanahitaji msaada zaidi hasa wa matibabu ili kuwapa faraja na wengi wao ni wazee waliotumikia nchi katika kuikomboa kwenye mapinduzi.

Hashim alisema wazee wengi wasiojiweza kutokana na maradhi na maisha duni, walipambana katika kuikomboa nchi kwenye mikono ya wakoloni na walipoteza nguvu na wengine kumwaga damu kwa ajili ya kuleta uhuru na amani ya Zanzibar.

Pia alisema serikali ya Zanzibar ina kila sababu ya kuwaenzi wazee na kuhakikisha wanawapa kipaumbele katika uamuzi hasa kwenye nyanja za maendeleo na yote yaliyofanyika hasa kwenye miundombinu na maeneo mengine wao ndio waliofanya kipindi cha ujana wao.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI
INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042,
DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 0782253676

## KUPOTEA KWA CHETI



HAMISI IBRAHIMU OMARY anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S0358-0041 kilichotolewa Baraza na Mitihani la Taifa kupitia SHIGHATINI SEKONDARI mwaka 2014. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: DAR/URA/RB/15077/2022.

## KUPOTEA KWA CHETI



SCOLASTICA AGUSTINO KASHAMAKULA anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S2120/0015 kilichotolewa Baraza na Mitihani la Taifa kupitia KATUMA SEKONDARI mwaka 2014. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: MBE/MBE/RB/434179/2019.

**WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAKAZI**
**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**
**WILAYA YA MASWA.**
**MAHALI MASWA.**
**MAOMBI RUFAA NA.63 YA MWAKA 2021**
**KATI YA**
**TELA SEBASTIAN ...............MWOMBAJI**
**DHIDI YA**
**JUMA GILYA ............MJIBU MAOMBI**
**WITO/TAARIFA**

**Kwa: JUMA GILYA POPOTE ALIPO KATIKA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA.**

Kwa kuwa mwombaji hapo juu amefungua Maombi dhidi yenu katika Baraza hili la wilaya ya Maswa.Maelezo ya madai yanaweza kupatika hapa Barazani.Unatakiwa kuleta hapa Barazani utetezi wako wa maandishi(WSD)kabla ya tarehe 01.02.2022.

Pia unajulishwa kuwa Maombi haya yamepangwa kutajwa siku ya tarehe 01.02.2022 saa 2;30 asubuhi mbele ya Mhe.J.T.Kaare Mwenyekiti,Baraza la Ardhi na Nyumba Wilaya-Maswa.

Na pia unafahamishwa kuwa iwapo utakadi wito huu na kushindwa kufika siku iliyopangwa,Baraza litalazimika kusikiliza Maombi haya upande mmoja na kutoa uamuzi dhidi yako.

**IMETOLEWA** kwa **MKONO** wangu na **MHURI** wa Baraza hili leo tarehe 06.01.2022

**J.T.KAARE**
**MWENYEKITI**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA(W)**
**MASWA**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

ATHANAS PAUL KIPETO ANATANGAZA kupotelewa na kadi ya GARI (TRAILER) mali ya ZH.POPPE LTD yenye namba za usajili T 267 BKS Injini namba AMT011103010 Kadi Namba 6331668 Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi taarifa ya polisi RB namba IRI/IRI/RB/14313/2022.

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

ABDULRAHMAN MUSTAFA ATHUMAN anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya FUSO yenye namba za usajili T 164 AKZ Lenye chases namba FK517K5201501. KADI namba.5981393. Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa polisi. Taarifa ya polisi RB. Namba IRI/KIL/RB/52192022

Magistrates Court (Approved Forms For the Primary Court)
**GN. NO 943(Contd.)**
**FOMU MADAI -3**
**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo Wilaya ya Moshi**
**Kituo cha Moshi Mjini Mkoa Kilimanjaro**
**Shauri la Madai / Ndoa Na 62, 2022**
**Jina la Mdai Lulu Charles Swai**
**Jina la Mdaiwa Fred Renatus Myinga**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**

**(Kanuni ya 18 kanuni za taratibu Madai katika Mahakama za Mwanzo)**
**Kwa: Fred Renatus Myinga**

Kwa kuwa Mdai/Wadai ameleta /Wameleta madai yake /yao kwamba (Eleza hapa habari za Madai )
Mdai anaomba mahakama itoe talaka hivyo fika mahakamani kujibu madai hayo
Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika mahakama hii tarehe 18 mwezi 01 mwaka 2022 saa 03:00 asubuhi kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashaidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.
**ANGALIZO:** Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini,Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya w ewe kuwepo.
**Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 10 mwezi 01 Mwaka 2022**

.................................................................
**HAKIMU**

**FOMU MIRATHI - 2**
**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya TEMEKE**
**Kituo cha JUMUISHI Mkoa DAR ES SALAAM**
**Usimamizi wa mirathi Na. 56/2022**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU SHABANI PAZI MWINYIGOGO**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOTOLEWA NA MSAFIRI SHABANI PAZI**
**TANGAZO**
**(Kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 2 Mwezi 2 Mwaka 2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
Imetolewa leo tarehe 11 Mwezi 1 Mwaka 2022.

**FOMU MIRATHI - 2**
**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya TEMEKE**
**Kituo cha JUMUISHI Mkoa DAR ES SALAAM**
**Shauri la Madai/Ndoa Na. 30/2021**
**Jina la mdai: YOSIA MELKEZEDECK ELIA**
**Jina la mdaiwa: SINCEA ANDREW MGENI**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(Kanuni 18 ya Kanuni za taratibu Madai Katika Mahakama za Mwanzo)**
**Kwa: SINCEA ANDREW MGENI**
**Kwa kuwa Mdai/Wadai ameleta/wameleta madai yake/yao kwamba**
**TALAKA**

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe 1 Mwezi wa 2 Mwaka 2022 saa 8:30 asubuhi kwa mujibu madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.
ANGALIZO: Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini, Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo.
Hati hii imetolewa kwa amri yangu na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 10 Mwezi wa 1 Mwaka 2022.

## KUPOTEA KWA CHETI



FARIDA ABEDI MALICK anatangaza kupotelewa kwa cheti cha chuo Makumira University cheti cha Shahada ya Utawala na Uhasibu kilichotolewa mwaka 2016
Yeyote atakaye kiona atoe taarifa kituo cha polisi.
Taarifa polisi: KIL/MOS/RB/10564/2022

## TANGAZO LA MNADA

**TAN-GLOBAL VENTURES COMPANY LIMITED** kwa idhini iliyopewa na **MAHAKAMA** itauza kwa mnada wa hadhara nyumba iliyo orodheshwa kwenye jedwali katika eneo husika:

| ACCOUNT NAME | PLOT NO |
|---|---|
| PAULINA MORIS MTONO | BLOCK NO “KV” 230 KIVUMBITIFU TANGA CITY |

**MASHARTI YA MNADA:**
1. Nyumba tajwa hapo juu itauzwa kwa mnada wa hadhara baada ya wiki mbili ya tangazo hili endapo mlengwa hatalipa madeni yake ndani ya muda huo.
2. Mnunuzi aliyeshinda anatakiwa kulipa asilimia ishirini na tano(25%) mara tu baada ya mnada kufungwa,na atakamilisha asilimia sabini na tano(75%) baada ya siku kumi na nne(14),Fedha hiyo isipolipwa ndani ya muda huo mnada utarudiwa bila kurudishiwa fedha ya awali.

**Mkurugenzi Mtendaji**
**Imetolewa leo tarehe 11/01/2022 na TAN-GLOBAL VENTURES CO.Ltd, S.L.P 612, TANGA,**
**abrahamshempemba@gmail.com**
**0715-752205, 0714-560080, 0692-693410**

## KUPOTEA KWA OFFER YA KIWANJA (LETTER OF OFFER)

Ndugu ALICE MWAKILASA MWAFYELA wa S.L.P.765, Mbeya anatangaza kupotelewa na barua ya toleo ya kiwanja namba 289 kitalu " P " kilichopo Machinjioni mkoani Mbeya. Atakayeiona barua ya toleo (letter of Offer) hiyo anaombwa arudishe Halmashauri ya Jiji la Mbeya S.L.P. 149,au aripoti kituo chochote cha polisi kilicho karibu.
TAARIFA YA POLISI:MBE/MBE/RB/536460/2021.

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA KYELA**
**LILILOPO KYELA**
**MAOMBI NA.11/2020**
**KADENA MWAKASYELE......................MWOMBAJI**
**DHIDI YA**
**KELVIN MWAMKINGA.................MJIBU MAOMBI 1**
**KAISI KALAMBO(Msimamizi wa mirathi ya marehemu ISSA KAISI).......MJIBU MAOMBI 2**
**EMANUEL MWAKIFUNA..............MJIBU MAOMBI 3**
**LILIAN JONAS GEORGE................MJIBU MAOMBI 4**
**WITO/KUITWA SHAURINI**
**KWA:**
**LILIAN JONAS GEORGE**

Fahamu kwamba,Kadena Mwakasyele amefungua shauri dhidi yako katika baraza hili.
Shauri limepangwa kutajwa tarehe 18/01/2022 saa 2:30 asubuhi mbele ya Mhe.B.J.Cyril Mwenyekiti wa Baraza.Unatakiwa kuleta utetezi wa maandishi ndani ya siku 21 tangu tarehe ya wito huu.
Nyaraka zinazohusu shauri hili zinzpatikana katika masjala ya Baraza la Ardhi na Nyumba la wilaya ya Kyela.
Unaamriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa wewe mwenyewe au mwakilishi anayeruhusiwa kisheria.
Kumbuka:Usipohudhuria siku hiyo,Baraza litatoa amri stahilivu ikiwa ni pamoja na kusikiliza shauri pasipo wewe kuwepo.
Amri hii imetolewa kwa mkono waqngu na mhuri wa baraza hili leo tarehe 20/12/2021.

**B.J.Cyril**
**Mwenyekiti**
**20/12/2021**

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**JUDICIARY**
**IN THE RM'S of njombe**
**AT NJOMBE**
**CIVIL CASE NO.04/2021**
**NMB BANK PLC...........PLAINTIFF**
**VERSUS**
**JOELY PATRICK MTWEVE.....DEFENDANT**
**SUMMONS TO FILE WRITTEN STATEMENT OF DEFENCE.**
**TO**
**JOELY PATRICK MTWEVE & MAVELINA DANISIUS MGENI**

WHERE AS the above named plaintiff has instituted a suit against you upon the claim the particulars of which are set out in annexed copy of the plaint.
YOU ARE HEREBY NOTIFIED that you must file your WRITTEN STATEMENT OF DEFENCE in duplicate within twenty one (21) days of services of this notice upon you.If there is more than one plaintiff,additional copies of your written statement of defence must be filed sufficient for service on each of the plaintiffs.If there are more defendants than one and the defence is not joint defence,you must file sufficient copies for service on each of the other defendants.
AND TAKE NOTICE that the case also has been fixed for order before HON.MLOWE magistrate on the 17th day of January,2022 at 08:00 o'clock in the morning.
Given under my hand and the seal of the court this 20th day of Dec,2021.

......................................
**Hon.Mlowe**
**RESIDENT MAGISTRATE**
**THE RESIDENT MAGISTRATES COURT**
**NJOMBE**

**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**MBEYA**
**KUITWA SHAURINI**
**SHAURI LA RUFAA JINAI NA. 77/2019**
**(Asilia Shauri la Hujuma Na.1/2018. Mahakama ya Hakimu Mkazi Mbeya)**
**JAMHURI...........................MRUFANI**
**DHIDI YA**
**KENEDY LUPEMBE SIMSOKWE…MJIBU RUFAA NA.1**
**MATRHEW ELIKANA MWANJALA...MJIBU RUFAA NA.2**
**SHABAN MKWICHE…………MJIBU RUFAA NA.3**
**KWA BWANA: 1. KENEDY LUPEMBE SIMSOKWE.**
**2. MATHEW ELIKANA MWANJALA**
**3. SHABAN MKWICHE**

**POPOTE MLIPO TANZANIA.**
Mnaamriwa na Mahakama hii kuhudhuria hapa Mahakama Kuu Kanda ya Mbeya, Tarehe 17/01/2022 siku ya Juma tatu Saa3:00 Asubuhi bila kukosa.
ELEWA KWAMBA Ukikosa kufika siku hiyo Shauri litasikilizwa upande mmoja bila nyinyi kuwepo na Uamuzi kutolewa.
Hati hii imetolewa kwa Amri yangu na Muhuri wa Mahakama leo hii Tarehe 25/10/2021.

**NAIBU MSAJILI**
**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**MBEYA**

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

SANLG WORLD WIDE INVESTMENT LIMITED ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI AINA SANL YENYE NAMBA ZA USAJILI MC 716 DAB KWA YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI TAARIFA YA POLISI KAH/TR /RB/19/022

OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji
THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

# Binadamu wa kwanza kupandikizwa moyo wa nguruwe



Daktari Bingwa wa Upasuaji, Bartley Griffith (kushoto), akiwa na David Bennett ambaye amefanyiwa upasuaji na kupandikizwa moyo wa nguruwe. **PICHA: BBC**

**Baltimore,** MAREKANI

MWANAMUME wa Kimarekani amekuwa binadamu wa kwanza duniani kupandikizwa moyo wa nguruwe, aliyebadilishwa vinasaba (GMO), katika upasuaji wa kwanza duniani

David Bennett (57), anaendelea vyema ikiwa ni siku ya tatu, baada ya upasuaji wa majaribio hayo uliofanyika katika mji wa Baltimore, wanasema madaktari.

Upandikizaji wa moyo huo, unachukuliwa kama matumaini ya kuyakoa maisha ya Bennett, ingawa haijawa wazi ni fursa ya kiasi gani aliyonayo, ili aishi maisha marefu.

"Ulikuwa ni upandikizaji wa kufanya au afe," Bennett alielezea siku moja kabla ya upasuaji.

"Ninafahamu kwamba ni jambo la kubahatisha, lakini ni chaguo langu la mwisho," aliongeza.

Madaktari wa Chuo Kikuu cha Maryland Kituo cha Tiba, walipewa idhini maalum na wasimamizi wa matibabu kuendelea na upasuaji huo, kwa misingi kwamba vinginevyo Bennet angekufa.

Hakuwa na uwezo wa kupandikiziwa moyo wa binadamu, uamuzi ambao mara nyingi huchukuliwa na madaktari wakati mgonjwa anapokuwa na afya duni sana.

Timu ya madaktari, iliyofanya upandikizaji huo, ilisema mafanikio hayo yamehitimisha miaka kadhaa ya utafiti na yanaweza kubadili maisha kote duniani.

Daktari wa Upasuaji, Bartley Griffith, alisema upasuaji huo utaileta dunia katika hatua moja ya kukaribia kutatua mzozo wa ukosefu wa kiungo cha mwili.

Watu 17 kwa siku hufariki Marekani, wakati wakisubiri kufanyiwa upasuaji wa kupandikizwa viungo, huku zaidi ya 100,000 wakiripotiwa kungojea upasuaji.

Uwezekano wa kutumia viungo vya wanyama kwa ajili ya kile kinachoitwa 'xenotransplantation' ili kufikia mahitaji, umekuwa ukifikiriwa kwa muda mrefu na matumizi ya mishipa ya moyo wa nguruwe, tayari limekuwa ni jambo la kawaida.

Oktoba, mwaka jana, madaktari wa upasuaji mjini New York, walitangaza kwamba wamefanikiwa kupandikiza figo ya nguruwe kwa binadamu.

Wakati huo, upasuaji ulikuwa ni jaribio la teknolojia ya hali ya juu zaidi kuwahi kufikiwa. Hata hivyo, ubongo wa mtu

Bennett, ana matumaini kuwa upandikizaji wake wa moyo wa nguruwe utamwezesha kuendelea na maisha yake.

Alikuwa amelala kitandani kwa wiki sita mfululizo, kabla ya kufanyiwa upasuaji na aliwekewa mashine ambayo ilimwezesha kuendelea kuishi baada ya kupatikana na maradhi yanayoua ya moyo.

"Natazamia kunyanyuka na kuondoka kitandani baada ya kupona," alisema wiki iliyopita.

Wiki hii, Bennett aliripotiwa kupumua mwenyewe huku akiendelea kufuatiliwa kwa karibu.

Lakini kile kitakachotokea baadaye hakijawa wazi. Nguruwe aliyetumiwa katika upandikizaji alifanyiwa mabadiliko ya vinasaba, ili kuondoa jeni kadhaa ambazo zingefanya kiungo hicho kikataliwe na mwili wa Bennet, linaripoti shirika la habari la AFP.

Griffith, alisema wanaendelea kumfuatilia kwa makini na kwa uangalifu mkubwa, huku mwanawe wa kiume, David Bennett Jr, akiliambia Shirika la Habari la Associated Press kwamba familia yao iko katika hali ya sintofamu wakati huu."Natambua ukubwa wa kile kilichofanyika na anatambua umuhimu wake."

"Hatujawahi kufanya hili kwa binadamu na ninapenda kufikiria kwamba tumempatia chaguo bora kuliko kile ambacho kingetokea kama angeendelea kupewa matibabu aliyokuwa akiyapata," alisema Griffith. Lakini iwapo ataishi kwa siku, wiki, mwezi au mwaka, sijui."

**BBC**


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA WAZIRI MKUU
KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU
WAKALA WA USALAMA NA AFYA MAHALI PA KAZI (OSHA)

MAADHIMISHO YA MIAKA 58
YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR



Dk. Hussein Ally Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi

Menejimenti na Wafanyakazi wa Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA) tunaungana na Mh. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Hussein Ally Hassan Mwinyi na Mh. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Wananchi wote kwa ujumla katika kuadhimisha Miaka 58 ya Mapinduzi matukufu ya Zanzibar.



Mh. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

"Usalama na Afya Mahali pa Kazi huongeza tija" OSHA inasimamia hilo

Occupational Safety and Health Authority
osha_tanzania_official
TanzaniaOsha
Osha online TV

SIMU YA BURE: 0800110091/2

Mamlaka ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA),
P.O Box 519, DAR ES SALAAM
Simu Na: +255- (0)22 -2760548/276055
Nukushi Na: (022) 27605 Barua pepe: info@osha.go.tz

# YANGA PRINCESS YAPOROMOKA LIGI KUU

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kuchapwa mabao 4-1 na watani zao wa jadi Jumamosi iliyopita, timu ya soka ya wanawake, Yanga Princess, imeporomoka kutoka nafasi ya tatu hadi ya sita kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara ikiwa kwenye raundi ya nne.

Wakati Yanga Princess ikishuka hadi kwenye nafasi ya sita, Simba Queens, imeendelea kuwa kileleni mwa soka tangu kuanza kwa ligi hiyo na sasa imefikisha jumla ya pointi 12 kwa mechi nne ilizocheza, huku ikiwa imepachika mabao 31 na kufungwa mawili, ikiwa haijatoka sare wala kupoteza.

**Yanga Princess, kabla ya kucheza na Simba ilikuwa kwenye nafasi ya tatu ikiwa na pointi saba, imebaki na pointi zake hizo, lakini ikiporomoka hadi nafasi ya sita, baada ya timu zingine kushinda kwenye mechi zao, huku yenyewe ikipoteza dhidi ya Simba Queens kwa mabao 4-1, Jumamosi iliyopita, Uwanja wa Benjamin Mkapa.**

Timu tishio kwenye ligi hiyo, Fountain Gate Princess, inaendelea kushika nafasi ya pili ikiwa na pointi 10 baada ya kuichapa Mlandizi Queens mabao 5-1, huku Alliance Girls ya Mwanza ikikaa kwenye nafasi ya tatu, ikiwa imefikisha pointi nane baada ya sare ya bao 1-1 dhidi ya Oysterbay Girls, kwenye nafasi ya nne ikikaa The Tigers Queens ikiwa na pointi saba, ilipoichapa Baobab Queens bao 1-0, na JKT Queens nayo ikienda mpaka kwenye nafasi ya tano kwa pointi saba, baada ya sare ya mabao 2-2 dhidi ya Ilala Queens.

Yanga Princess ambayo pia ina pointi saba, inazidiwa na timu hizo mbili kwa tofauti ya mabao ya kufunga na kufungwa.

KUJIFUA...



Wachezaji wa timu ya vijana, ya mpira wa Kikapu, wakifanya mazoezi katika viwanja vya Jakaya Kikwete Jijini Dar es Salaam. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *KMKM sasa wajipanga kwenye ligi*

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

TIMU ya KMKM imesema baada ya kutofanikiwa kufanya vizuri katika michuano ya Kombe la Mapinduzi hivi sasa wanaendelea na kujipanga kuelekea michezo ya Ligi Kuu ya Zanzibar.

KMKM ni timu pekee ya ambayo wadau Wazanzibar walikuwa na matumaini huwenda akitinga hatua ya nusu fainali.

Akizungumza na gazeti hili Kocha wa Timu ya KMKM, Ame Msimu, alisema hivi sasa wanajikita na kuendelea na mipango yao ya kuusaka ubingwa katika Ligi Kuu ya Zanzibar ambayo bado inaupinzani mkali.

Timu ya KMKM ambao ndio vinara wa Ligi Kuu ya Zanzibar akiwa na alama 33 ikishinda michezo 9 na sare 6 na hawakuwahi kufungwa katika michezo 15 waliyocheza.

Alisema kuwa kupitia michuano hiyo ya Kombe la Mapinduzi ambayo wamebahatika kucheza na timu yenye uzoefu mkubwa katika michuano ya ndani na ile ya kimataifa hivyo watatumia uzoefu walioupata katika michezo ya ligi.

"Tunajiandaa kuelekea michezo ya Ligi Kuu, tupo katika mbio za kuutaka ubingwa wa Zanzibar, na kama mnavyojua ligi yetu ni ngumu sana kila timu inapambana kupata mafanikio ikiwamo kutwaa taji," alisema.

Hata hivyo alisema wamewapa mapumziko mafupi wachezaji wa timu hiyo kwa ajili ya kujiandaa na michezo ya Ligi Kuu ya Zanzibar mzunguko wa lala salama.

## Muumin asaka vimwana

**Na Sabato Kasika**

MWIMBAJI nyota wa muziki wa dansi, Mwinjuma Muumin, amesema anasaka wasanii wa kike wa muziki wa kizazi kipya na taarabu ili awashirikishe kwenye moja ya nyimbo zake mpya.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Muumin alitaja wasanii anaowasaka kuwa ni Nandy, Rubby, Lady Jay Dee, Zuchu na Isha Mashauzi, kwamba akipata mmojawapo, atamshirikisha.

"Ninataka kufikia mwishoni mwa mwezi huu, nirekodi nyimbo mbili mpya ambazo ni 'Usiniache na Njoo Kwangu', ambazo mmojawapo ninataka kushirikisha wasanii wa kike," amesema Muumin.

Mwanamuziki huyo ambaye ni mmiliki wa Special Band, amesema, lengo lake ni kupata vionjo tofauti kutoka kwa wasanii wa muziki wa kizazi kipya ili kuboresha muziki wake.

"Wasanii wa muziki wa kizazi kipya wana umuhimu wake, kutokana na kwamba wana mashabiki wengi, hivyo kuwashirikisha kwenye nyimbo zangu kunaweza kuongeza vionjo katika dansi," amesema.

## Kipa Namungo amvulia kofia Sakho

**Na Sada Akida,** ZANZIBAR

KIPA namba moja wa Namungo FC, Jonathan Nahimana, amenyoosha mikono kwa nyota wa Simba, Pape Ousmane Sakho kwa kudai alikuwa hatari kwa upande wao.

Kauli ya kipa huyo ni baada ya nyota huyo kufunga bao la pili katika nusu fainali ya Mapinduzi na Namungo FC kukubali kichapo cha mabao 2-0 dhidi ya Simba, mchezo uliopigwa juzi saa 2:00 usiku uwanja wa Amaan, Visiwani Unguja.

Akizungumza na gazeti hili jana, Nahimana alisema wanacheza na Simba mara kadhaa mchezo unakuwa wa ushindani na kutopata wakati mgumu kutoka kwa wapinzani wao Simba.

Alisema mchezo huu amepata wakati mgumu sana hasa kwa ubora na kiwango kilichoonyesha na Sakho amekuwa hatari kwa upande wake na bora katika safu ya ushambuliaji ya Simba.

Alisema Sakho ndio mchezaji ambaye alikuwa hatari kwa upande wa Simba na kustahili kuwa mchezaji bora wa mchezo huu. Kipa huyo alisema wanapokea matokeo hayo wanarudi Dar es Salaam kwenda kujipanga na michezo yao ya Ligi Kuu Tanzania Bara.

## ZISIKUPITE

### RUDIGER ATAJWA MADRID

MLINZI wa Chelsea, Antonio Rudiger mwenye umri wa miaka 28, ambaye mkataba wake unamalizika msimu wa joto bado hajasaini mkataba mpya na mabingwa hao wa Ulaya, na ameripotiwa kuwaniwa na Real Madrid. ***(Football London)***

### CAVANI KUBAKI

MSHAMBULIAJI wa Uruguay, Edinson Cavani mwenye umri wa miaka 34, ameahidi kujitolea kwa Manchester United kwa muda wote uliosalia wa msimu huu baada ya mazungumzo na kocha Ralf Rangnick. ***(Mirror)***

### ORIGI HUYO LAZIO

MKURUGENZI wa michezo wa Lazio, Igli Tare ameanzisha mazungumzo na Liverpool kumhusu mshambuliaji wa Ubelgiji, Divock Origi, huku wekundu hao wakiwa tayari kumuuza nyota huyo mwenye umri wa miaka 26 kwa kuhofia kumpoteza kwa uhamisho wa bure Juni. ***(LazioNews24)***

### NEVES AWANIWA

KLABU ya Manchester United imedhamiria kumsajili kiungo wa Wolverhampton Wanderers na Ureno, Ruben Neves mwenye miaka 24,mwezi huu. ***(The Sun)***

### NYOTA KURUHUSIWA LIVER

LIVERPOOL huenda ikamruhusu mlinzi wa Wales, Neco Williams mwenye miaka 20, na beki Muingereza, Nathaniel Phillips mwenye miaka 24, kuondoka klabu hiyo katika dirisha la uhamisho wa Januari. ***(Sky Sports)***

### RAMSEY KUONDOKA

KIUNGO wa kati wa Wales, Aaron Ramsey mwenye miaka 31, anajiandaa kuondoka Juventus, ambako analipwa euro 325,000 kwa wiki. ***(Sky Sports)***

### DIGNE KUONDOKA

KIUNGO wa Everton, Lucas Digne mwenye umri wa miaka 28, huenda akahamia klabu nyingine ya Ligi Kuu England. Hata hivyo Newcastle sio chaguo la mchezaji huyo wa kimataifa wa Ufaransa. ***(Fabrizio Romano via Twitter)***

### DEST SASA KUMRITHI DIGNE

CHELSEA wanatafakari uwezekano wa kumnunua beki wa Barcelona na Marekani, Sergino Dest mwenye umri wa miaka 21, kama mbadala wa Lucas Digne. ***(Daily Star)***


### GOMEZ MALI YA VILLA

ASTON Villa hawana 'nafasi' ya kumsajili kiungo wa Liverpool na Uingereza, Joe Gomez. ***(Athletic)***

### HAALAND KUFANYA UAMUZI

KLABU ya Borussia Dortmund watafanya uamuzi kuhusu hatma ya mshambuliaji wa Norway mwenye umri wa miaka 21, Erling Braut Haaland 'wiki chache zijazo'. ***(Daily Mail)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# RANGNICK: MCTOMINAY ATAKUWA NAHODHA

●●● Amsifia baada ya kufunga bao na kuiwezesha Man kusonga mbele FA na...

**MANCHESTER,** England

RALF Rangnick anaamini kwamba, Scott McTominay anaweza kuwa nahodha wa Manchester United katika "miaka kadhaa" na amemsifu David de Gea baada ya ushindi wa 1-0 dhidi ya Aston Villa kwenye kombe la FA.

McTominay alifunga bao pekee katika pambano hilo la raundi ya tatu pale uwanja wa Old Trafford Jumatatu, akiunganisha kwa kichwa mpira wa pasi uliotoka kwa Fred dakika ya saba.

**Hiyo ilitosha kwa Mashetani Wekundu hao kuwapeleka raundi ya nne ambapo watacheza dhidi ya Middlesbrough.**

Huku kukiwa na machafuko katika chumba cha kubadilishia nguo cha United kufuatia kichapo cha 1-0 kutoka kwa Wolves, kulikuwa na ahueni kwa Rangnick baada ya ushindi huo.

Alipoulizwa kuhusu mchango wa McTominay, Rangnick aliambia BBC Sport: "Yeye ni mvulana kutoka akademi, nguvu zake ni za ajabu. Sasa pia anaanza kufunga mabao na pia ujuzi fulani wa uongozi.

"Sitashangaa ikiwa katika miaka kadhaa atakuwa nahodha wa timu hii."

Aliongeza: "Lazima tuimarishe timu kuwa timu safi na hiyo ilikuwa nyingine leo (juzi) lakini bado David de Gea alikuwa bora kwangu tena leo (juzi)."

SportPesa | LIVE IN PLAY

MECHI KALI
BARCELONA
VERSUS
REAL MADRID
1 | 3.53
X | 3.53
2 | 1.97

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
18+
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# BARCA WAMSAJILI TORRES



**BARCELONA,** Hispania

BARCELONA hatimaye imefanikiwa kumsajili mchezaji mpya Ferran Torres baada ya kukubaliana mkataba mpya na Samuel Umtiti, ambayo inashuhudia mshahara wa Mfaransa huyo ukipunguzwa kwa muda.

Barca ilimsajili Torres kutoka Manchester City mwezi uliopita kwa dili ambalo huenda likagharimu Euro milioni 65, lakini kutokana na ugumu wa kifedha wa klabu hiyo, hawakuweza kumsajili.

Kiwango cha mshahara wa Blaugrana hao msimu huu kiliwekwa kuwa euro milioni 97 pekee, punguzo la euro milioni 280 kutoka msimu wa 2020-21 kutokana na utendaji wao wa kifedha.

Ingawa mkopo wa hivi majuzi wa benki uliripotiwa kufanikisha usajili wa Torres, klabu hiyo imelazimika kufanya ubunifu katika matumizi yake ya fedha, ili kuhakikisha anastahili kucheza La-Liga.

Maisha ya Umtiti Barca yameathiriwa na majeraha tangu ajiunge nayo akitokea Lyon mwaka 2016.

Lakini licha ya masuala hayo na ripoti zinaonyesha kuwa Barca walikuwa wakijaribu kumtoa Umtiti katika klabu hiyo, Mfaransa huyo amepewa mkataba mpya na anashukuru kwa kusaidia kumsajili Torres.

Taarifa ilisema: "Mchezaji wa Barcelona Samuel Umtiti amefikia makubaliano ya kuongeza mkataba hadi Juni 30, 2026.



## Ronaldo ameichoka Man U

**MANCHESTER,** England

CRISTIANO Ronaldo amemwambia wakala wake Jorge Mendes kwamba anataka klabu mpya kutokana na kuchoka kucheza Manchester United.


Kwa mujibu wa mtandao wa michezo wa Sport nchini Hispania, uhusiano mzuri wa Mendes na Rais wa Barcelona Joan Laporta pamoja na uhitaji wa magoli wa Kocha Xavi Hernandez unafanya kuwapo kwa uwezekano wa Ronaldo kuhamia Nou Camp majira ya kiangazi.

Mendes atawasilisha jina la Ronaldo kwenye meza ya Barcelona kuhusiana na kile kitakuwa uhamisho wa kusisimua wa nyota huyo wa zamani wa Real Madrid.

Ronaldo alijiunga na Manchester United akitokea Juventus msimu huu saa chache baada ya uvumi kuenea alikuwa mbioni kujiunga na Manchester City.

CHEZA USHINDE KASINO

JISAJILI CHEZA SHINDA



# MUSTAPHA AWAOMBA RADHI MASHABIKI YANGA

**Na Dennis Fussi**

BEKI wa kushoto wa Yanga, Yassin Mustapha, amewaomba msamaha wanachama na mashabiki wa timu hiyo kwa kukosa mkwaju wa penalti wakati wa mchezo wa nusu fainali ulioitoa timu yake kwenye mashindano ya Kombe la Mapinduzi.

Yanga iliyotolewa kwa changamoto ya mikwaju ya penalti tisa kwa nane kwenye nusu fainali ya Kombe la Mapinduzi dhidi ya Azam FC juzi.

Akizungumza baada ya mchezo huo, Mustapha amesema tukio hilo limemuumiza na kumnyima furaha, sababu anajiona kama msaliti.

"Ukweli ni kwamba, nimepoteza furaha najiona kama nimewasaliti wenzangu kutokana na mikakati tuliyokuwa tumejiwekea kwenye mashindano haya ila naomba wanachama na mashabiki wanisamehe sikutarajia kufanya kile kilichotokea," amesema Yassin.

Katika mchezo huo wa nusu fainali ya kwanza kwenye uwanja wa Amaan Zanzibar Yanga siyo tu imetolewa bali pia imevuliwa ubingwa baada changamoto ya penalti 9-8 dhidi ya Azam, kufuatia timu hizo kutoka suluhu katika muda wa kawaida.



Mchezaji wa Timu ya Stony City (kulia), akimiliki mpira huku akizongwa na mchezaji wa Ijumaa FC kwenye mchezo wa robo fainali ya michuano ya kuwania mbuzi katika Uwanja wa Dadii Kivule jijini Dar es Salaam juzi, Stony City ilishinda kwa mikwaju ya penalti 5-4. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Kotei wa Simba naye anukia DTB*

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI ikitarajia kucheza mechi yake ya kumaliza mzunguko wa kwanza wa Ligi ya Championship siku ya Ijumaa dhidi ya Kitayosce, klabu ya DTB iko mbioni kumsajili kiungo mkabaji wa zamani wa klabu ya Simba, James Kotei.

Ofisa Mtendaji Mkuu, Muhibu Kanu, ameshindwa kukubali au kukataa kumtaka kumsajili mchezaji hiuyo, lakini amesema Kotei raia wa Ghana, tayari yupo nchini na ametembelea kwenye kambi ya klabu hiyo, huku akiongeza kuwa masuala ya usajili atayazungumza baada ya kumalizika kwa mzunguko wa kwanza wa ligi hiyo ambayo timu mbili za mwanzo zitapanda moja kwa moja Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao.

"Kotei yupo hapa nchini, na amefika kwenye kambi yetu, amekuja kutusalimia na kusalimia wenzake. Kuna mchezaji mwenzake raia wa Ghana, wameshawahi kucheza naye wakiwa kwenye klabu ya Simba Nicolaus Gyan," alisema Kanu.

Alisema ni kweli wako kwenye mchakato wa kuongeza baadhi ya wachezaji kipindi cha dirisha dogo, lakini asingependa kuweka wazi majina yao.

"Kipindi hiki nisingeweza kuweka wazi kwa sababu bado tuna wachezaji wengine wanacheza, Ijumaa tuna mechi ya kumalizia mzunguko wa kwanza dhidi ya Kitayosce, sasa mchezaji wetu yoyote anayecheza nafasi ya kiungo mkabaji akisikia kuna mchezaji anakuja, itakuwa si vizuri," alisema.

Hata hivyo, habari zinasema kuwa kwa asilimia kubwa, Kotei atakuwa mmoja wa wachezaji waliowahi kucheza Ligi Kuu kuichezea DTB inayoongoza Ligi Kuu, iliyosheheni wachezaji wengi wa kigeni akiwamo Amissi Tambwe anayeongoza kwenye kufumania nyavu.

SPORTPESA APP

PAKUA APP YETU, BET LEO UWE MILIONEA

MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMATANO - 12/01/2022

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 15:00 | 3696 | Bisha FC vs Al Orubah | 3.85 | 3.15 | 2.07 |
| 15:30 | 1112 | Ermis Aradippou vs EN Paralimni | 2.33 | 3.33 | 2.70 |
| 15:30 | 3258 | PO Xylotymbou vs Olympias Lympia | 1.85 | 3.33 | 3.86 |
| 15:30 | 3442 | Achyronas Liopetriou vs Nea Salamis | 4.72 | 4.05 | 1.56 |
| 15:30 | 4732 | Onisilos Sotira FC vs Karmiotissa | 2.45 | 3.27 | 2.59 |
| 16:00 | 1497 | Kalamata FC vs Irodotos | 1.12 | 6.00 | 23.24 |
| 16:00 | 1802 | Tunisia vs Mali | 2.61 | 2.86 | 2.96 |
| 16:00 | 1853 | Olympiakos Volos vs PAOK Thessaloniki B | 2.73 | 3.07 | 2.45 |
| 16:00 | 2312 | SKODA Xanthi vs Panserraikos | 1.19 | 5.20 | 14.43 |
| 16:00 | 2504 | Karaiskakis vs Kallithea FC | 4.71 | 3.22 | 1.73 |
| 16:00 | 2932 | AEK Athens B vs Levadiakos | 6.57 | 3.62 | 1.49 |
| 16:00 | 3352 | Kifisias vs Rhodos FC | 1.96 | 3.09 | 3.76 |
| 16:00 | 3395 | Thesprotos vs Olympiacos Piraeus B | 2.75 | 3.04 | 2.46 |
| 16:00 | 3601 | Almopos Arideas vs AE Larissa | 5.95 | 3.41 | 1.57 |
| 16:00 | 3940 | Diagoras FC vs Kissamikos | 3.33 | 2.80 | 2.26 |
| 16:00 | 4678 | Pierikos Katerini vs PO Triglias | 3.66 | 3.33 | 1.90 |
| 16:00 | 5257 | Anagennisi Karditsas vs FC Veria | 2.47 | 2.95 | 2.81 |
| 16:00 | 5478 | Ergotelis vs O F Ierapetras | 1.66 | 3.34 | 5.03 |
| 16:00 | 5514 | AE Asteras Vlachioti vs APS Zakynthos | 1.18 | 5.40 | 15.43 |
| 16:00 | 5717 | Panathinaikos B vs Egaleo Athens | 2.93 | 2.79 | 2.50 |
| 17:00 | 1967 | Delhi Dynamos FC vs Kerala Blasters FC | 5.39 | 4.33 | 1.46 |
| 17:40 | 2026 | Al Khaleej Club vs Najran SC | 2.02 | 3.30 | 3.80 |
| 17:45 | 5913 | AL Adalh vs Jeddah Club | 1.70 | 3.65 | 5.20 |
| 18:00 | 4973 | Villarreal CF W vs Atletico Madrid W | 12.53 | 6.75 | 1.15 |
| 18:00 | 5150 | GIL Vicente U19 vs Feirense U19 | 1.34 | 4.83 | 6.76 |
| 18:00 | 5164 | SD Eibar W vs Levante W | 5.78 | 4.43 | 1.43 |
| 18:15 | 2355 | PAOK vs Panetolikos | 1.27 | 5.34 | 9.69 |
| 18:15 | 2881 | Apollon Smyrnis vs OFI Crete | 2.57 | 3.07 | 2.77 |
| 18:30 | 3445 | Al Ahli Doha SC vs Umm-Salal SC | 2.70 | 3.28 | 2.35 |
| 18:30 | 3878 | Varzim vs Sporting Farense | 3.23 | 3.18 | 2.17 |
| 18:30 | 4008 | Qatar SC vs Al-Shamal | 1.39 | 4.35 | 6.58 |
| 19:00 | 3027 | Sevilla FC W vs Rayo Vallecano W | 1.36 | 4.72 | 6.56 |
| 19:00 | 4261 | Mauritania vs Gambia | 2.52 | 2.97 | 2.97 |
| 19:30 | 4030 | Valencia W vs Real Sociedad W | 7.13 | 4.82 | 1.33 |
| 19:30 | 5695 | Atalanta vs Venezia | 1.29 | 5.32 | 8.87 |
| 20:00 | 5728 | Santos Laguna U20 vs Tigres U20 | 1.83 | 3.48 | 3.77 |
| 20:30 | 2195 | Deportivo Alaves W vs Madrid Ccf W | 2.23 | 3.57 | 2.70 |
| 20:30 | 5685 | Maccabi Netanya vs Hapoel Beer Sheva | 3.43 | 3.33 | 1.97 |
| 21:00 | 5774 | Maccabi Haifa vs Beitar Jerusalem | 1.28 | 5.17 | 7.85 |
| 21:30 | 4847 | Athletic Bilbao W vs Real Betis Balompie W | 1.64 | 3.95 | 4.24 |
| 21:45 | 4576 | Rio Ave vs Tondela | 2.56 | 3.14 | 2.56 |
| 22:00 | 2381 | Equatorial Guinea vs Ivory Coast | 14.85 | 5.15 | 1.24 |
| 22:00 | 3374 | Barcelona vs Real Madrid | 3.53 | 3.53 | 1.97 |
| 22:00 | 4183 | Real Madrid W vs Tenerife Sur W | 1.43 | 4.36 | 5.81 |
| 22:00 | 4574 | Peralada CF vs CE Manresa | 2.24 | 3.25 | 3.30 |
| 22:45 | 3778 | West Ham vs Norwich City | 1.28 | 5.60 | 10.00 |
| 22:45 | 3994 | Tottenham vs Chelsea | 2.63 | 3.33 | 2.53 |
| 22:45 | 4329 | Crewe vs Charlton | 3.44 | 3.34 | 2.04 |
| 23:00 | 2220 | Inter vs Juventus | 1.78 | 3.79 | 4.29 |
| 23:45 | 3712 | FC Vizela vs Porto | 10.57 | 5.19 | 1.23 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Jumatano Januari 12, 2022

Nipashe




Rangnick: McTominay atakuwa nahodha

UKURASA 21



Mlinzi wa Timu ya Simba, Shomari Kapombe, akiwania mpira dhidi ya mchezaji wa Namungo FC kwenye mchezo wa nusu fainali ya Kombe la Mapinduzi juzi, Uwanja wa Amaan mjini Zanzibar. **PICHA; SIMBA**

## Pablo akunwa na kiwango Simba

**Na Saada Akida,** ZANZIBAR

KOCHA Mkuu wa Simba, Pablo Franco, amesema amefurahishwa kuona mpira wa kuvutia kutoka kwa vijana wake kwenye mchezo wa nusu fainali ya Kombe la Mapinduzi dhidi ya Namungo FC.

Simba iliibuka na ushindi wa 2-0 kwenye mchezo huo na itacheza na Azam FC, kwenye fainali itakayopigwa kesho Uwanja wa Amaan, Zanzibar.

Pablo alisema mchezo dhidi ya Namungo ulikuwa wa kiufundi na kimbinu ulikuwa mzuri na wachezaji wake wamepambana na kupata matokeo mazuri. Alisema wanasahau matokeo hayo na wanaenda kujipanga kuhakikisha wanafanya vizuri katika mchezo wao wa fainali na kutwaa ubingwa wa Mapinduzi.

"Azam FC ni timu nzuri na ana imani utakuwa wa ushindani mkubwa, kutokana na ubora wa wapinzani wetu tunaenda kujiimarisha zaidi ili kufikia malengo," alisema Pablo.

Mtendaji Mkuu wa Simba, Barbara Gonzalez, alisema malengo yao ni kutafuta ushindi katika kila mechi na sasa wanajipanga kwa mchezo wa fainali dhidi ya Azam FC.

Alisema wachezaji wamekituma na kufanikiwa kutinga nusu fainali dhidi ya Namungo FC na kucheza mpira biriani ambao waliukosa kwa muda mrefu.

"Wachezaji wamecheza ule mpira ambao tuliukosa muda na sasa umerudi, tumeweka mikakati ya kuhakikisha tunaenda kupambana na kutwaa ubingwa wa Mapinduzi," alisema Barbara.

Alisema kuhusu usajili wataweka wazi siku ya mwisho ya kufunga dirisha la usajili kwa kuweka wazi majina ya wachezaji waliowasajili kuongeza nguvu.

# Kaze: Azam walistahili ushindi

**Na Faustine Feliciane**

### ●●● Asema walikamatwa zaidi kwenye dimba la kati, wajipanga Ligi Kuu na...

KOCHA msaidizi wa Yanga aliyeisimamia timu hiyo kwenye michuano ya Kombe la Mapinduzi Zanzibar, Cedrick Kaze, amekiri kuwa wapinzani wao Azam walistahili ushindi walioupata baada ya kucheza vizuri ndani ya dakika 90 kwenye mchezo wa nusu fainali ya michuano hiyo juzi jioni.

**Kaze akizungumza na gazeti hili jana alisema kwenye mchezo huo wa juzi wapinzani wao walikuwa vizuri zaidi eneo la katikati ambalo liliwasaidia sana kumiliki mpira.**

"Tumekubali kuwa tumetolewa, nawapongeza sana Azam walikuwa vizuri sana eneo la katikati la uwanja na walicheza vizuri kwa ujumla na walistahili kusonga mbele," alisema Kaze.

Aidha, kocha huyo raia wa Burundi alitoa ufafanuzi wa maamuzi yake ya kumtoa golikipa aliyecheza kwa karibu dakika zote za mchezo huo Aboutwalib Mshery na kuingia Erick Johora zikiwa zimebaki dakika za nyongeza.

Kaze alisema mabadiliko hayo yalikuwa ya kawaida na ya kiufundi kutokana na alichokiona mazoezini kwenye mazoezi ya mikwaju ya penati.

"Ni mabadiliko ya kawaida tu, Johara alifanya vizuri sana kwenye mazoezi, tulifanya mazoezi ya penalti na akaonekana kuwa vizuri ndio msingi wa mabadiliko yale," alisema Kaze.

Aidha, alisema kwa sasa wanarejea Tanzania Bara kujipanga kwa michezo ya Ligi Kuu na michuano ya Kombe la Shirikisho la Azam.

Alisema michuano ya mwaka huu ya Mapinduzi kwao imeishia hapo na wanarejea kwa nguvu kwenye michuano mingine.

Azam sasa itakabiliana na Simba kesho kwenye mchezo wa fainali ya michuano hiyo, baada ya wekundu hao kufuzu hatua hiyo kwa kuitupa nje Namungo FC kwa mabao 2-0 kwenye mchezo wa pili wa nusu fainali uliochezwa juzi usiku.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >